# Nipashe

Jumatano Juni 23, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580620

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Dembele aondolewa Euro 2020**

UKURASA 20

**Mapya** 'house girl' adaiwaye kunyonga mtoto wa bosi wake

UKURASA 3



**Mbunge** wa CCM adai mshahara wa wabunge 'kiduchu'

UKURASA 4



# Kodi majengo kwa Luku yawekwa sawa

UKURASA 2


## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**KIHONGOSI KATIBU MKUU MPYA UVCCM**

KAMATI Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM)...

UKURASA WA 4

**AJALI YA BARABARANI ILIVYOUA TISA MORO**

MADEREVA wawili kati ya watatu wa magari yaliyopata ajali iliyotokea eneo...

UKURASA WA 5

**AVEVA, WENZAKE KUJITETEA JUNI 29**

RAIS wa zamani wa Klabu ya Simba, Evans Aveva, na viongozi wenzake...


## Tahadhari corona III yatolewa kila kona

UKURASA 3 & 17



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (kulia), akiwahamasisha wafanyabiashara kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona kwa kuvaa barakoa na kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni, alipotembelea mnada wa Tinde, wilayani huo, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: MARCO MADUHU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




# Vigogo TRA matatani rushwa ya mil. 200/-

UKURASA 2


**MICHEZO** SARPONG, DUBE SHIDA FA YANGA, AZAM UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, akihitimisha hoja ya Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2021/2022, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kodi kwa Luku yawekwa sawa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SERIKALI imetegua kitendawili kuhusu uamuzi wake wa kutaka ukusanyaji wa kodi za majengo ufanyike kwa kutumia mfumo wa ununuzi na utumiaji wa umeme kupitia mashine za Luku, ikisema kodi hiyo haitamhusu mpangaji, bali mmiliki wa nyumba.

Akifafanua kuhusu utozaji wa kodi hiyo utakaoanza siku saba zijazo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema bungeni jana kuwa hakuna nyumba ambayo ina mita ya umeme, haihusiani na mmiliki wake.

Kuhusu nyumba za vijijini za nyasi, Waziri Mwigulu, alisema watu hao hawatahusika katika ulipaji wa kodi hiyo na wala hawatatoza kodi hiyo kutokana na matumizi ya umeme kwa sababu kufanya hivyo kutaongeza gharama za uzalishaji.

Kutokana na makato hayo, aliwataka Watanzania kutoiogopa teknolojia kwa kuwa imeletwa ili kurahisisha ufanyaji wa mambo.

Alisema wenzao wanaoshughulika na umeme pamoja na wanaoshughulika na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), wamewahakikishia kwamba mambo yote yatakwenda kwa programu.

"Leo hii wametuhakikishia kuwa wanao uwezo wa kuitisha mita zote wakajua na mtumiaji anatumia kiwango gani.

"Tulipohakikishiwa hayo, tukajua ni jambo ambalo litafanyika kwa mpango mahususi," alisema.

Juni 10 mwaka huu, wakati akiwasilisha makadirio bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, waziri huyo alisema:

"Kila mita ya umeme ina uhusiano na mmiliki wa jengo na kwa kuwa sheria ya kodi ya majengo inataka kodi hiyo ikusanywe kwa mmiliki au mtumiaji wa jengo, ninapendekeza kodi ya majengo ya kiwango cha Sh. 1,000 kwa mwezi kwenye nyumba za kawaida zenye mita moja na itakatwa kwenye ununuzi wa umeme.

"Aidha, ninapendekeza kiwango cha Sh. 5,000 kwa mwezi kwa kila ghorofa au apartment zenye mita moja, itakatwa kwenye ununuzi wa umeme (Luku). Serikali itaweka utaratibu kwenye nyumba za kawaida na za ghorofa zinazochangia mita moja na zinazotumia mita zaidi ya moja."

**KODI YA LAINI**

Kuhusu Kodi ya Laini ya Simu, Dk. Mwigulu alisema kuna watumiaji wasiopungua milioni nane wa viwango vya mwanzo ambayo matumizi yao hayazidi Sh. 1,000 na kwamba matumizi hayo yanakua hadi watumiaji wanaotumia Sh. 100,000 na kuendelea.

Alisema watumiaji wa Sh. 100,000 na kuendelea si wengi na kuwa wako kwenye zaidi 60,000.

Alisema kwa hiyo watumiaji watakaoweka Sh. 1,000 kwenda chini watakatwa Sh. tano (5), pale watakapoweka Sh. 7,500 hadi Sh. 10,000 watakatwa Sh. 76, anayeweka muda wa Sh. 50,000 atakatwa Sh. 186 na Sh. 100,000 atakatwa Sh. 225.

Kuhusu makato kwenye miamala ya fedha, Dk. Mwigulu alisema miradi ya kimkakati kama ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere na reli na kwamba ili ikamilike inahitaji zaidi ya Sh. trilioni 22.

Alisema fedha hizo zitaendelea kutumika wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo, huku serikali ikitafuta fedha sehemu nyingine ikiwamo mikopo yenye masharti nafuu.

"Niwaombe tunazingatia mambo yanayotukabili mbele yetu. Mfumo wa kodi wa kwetu ulivyo hadi sasa ukiondoa kodi za moja kwa moja, huu mzigo unaangukia kwa watu wachache," alisema.

Alisema hadi sasa walipakodi wakubwa ni 504 na kwamba Watanzania walioandikishwa katika orodha ya walipa kodi ni milioni 3.1.

"Kama ukiwa na ukwasi wa Sh. milioni 15, ukatozwa Sh. 10,000 kuna tabu gani kuijenga nchi yako?" Dk. Mwigulu alihoji.

Kuhusu kuziwekea uzio fedha zinazokusanywa, Dk. Mwigulu alisema fedha zitakazokusanywa nyingi ziko katika mifuko.

**SAMATTA, MOBETO**

Waziri Mwigulu aliwatangaza bungeni mabalozi wapya wa kodi nchini kuwa ni mchezaji wa kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta anayeichezea klabu ya Fenerbahce ya Uturuki.

Balozi mwingine wa kodi nchini kwa sasa ni mwanamitindo na msanii wa Bongo Fleva, Hamisa Mobeto.

## Vigogo TRA matatani rushwa ya mil. 200/-

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amebainisha kubaini viashiria vya rushwa kwenye Mamlaka ya Mapato (TRA) katika kuwakadiria kodi wafanyabiashara.

Alitoa kauli hiyo bungeni jana wakati ahitimisha mjadala kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/22 na Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22.

Dk. Nchemba aliweka wazi kuwa amebaini baadhi ya maofisa wa TRA walilazimisha kupewa rushwa ya Sh. milioni 200 ili kumpunguzia makadirio ya kodi mfanyabiashara mmoja kutoka Sh. milioni 400 hadi Sh. milioni 320. Waziri huyo alisema tayari alishaelekeza suala hilo kushughulikiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Mbali na uchunguzi wa taasisi hiyo, Dk. Nchemba alisema ameshamwagiza Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, kuchukua hatua mara moja dhidi ya maofisa hao. Alisema suala hilo linavuruga taswira ya serikali na ndiyo maana ameipeleka kesi hiyo kwa vyombo vya dola.

"Kwa mfano tulikuwa na kesi moja hivi juzi, kuna mtu mmoja alienda akakadiriwa Sh. milioni 400. Alivyokadiriwa Sh. milioni 400, yule aliyemkadiria akamwambia alete Sh. milioni 200 za kwao wale wakadiriaji, akataa.

"Alivyokataa ilikuwa tarehe 23 mwezi Novemba mwaka 2020, alivyokataa alikadiriwa kwa barua kwamba makadirio yako ni Sh. milioni 400, akaambiwa alete 200 (Sh. milioni 200), alivyosumbuka sumbuka, akaambiwa 'unajifanya mjanja?'

"Tarehe 27 kutoka tarehe 23 yaani siku nne baadaye, akakadiriwa Sh. bilioni 2.5, hiyo ilikuwa ni tarehe 27 Novemba 2020, alivyokadiriwa hii sasa akaenda akaongea nao, kwamba ule mpango basi nimeshakubali, akatanguliza Sh. milioni 100.

"Alivyotanguliza Sh. milioni 100, tarehe 3 Desemba ikashushwa ile kutoka Sh. bilioni 2.5 ikarudi milioni 320. Maana yake nini kama siyo rushwa?

"Nimewapelekea kumbukumbu hii vyombo vya dola, vitafanya kazi yake na wale watu (maofisa) nimeelekeza Kamishna achukue hatua," alisema.

Waziri huyo aliweka wazi kuwa ni suala ambalo linawapa shida na kwa sasa wanalifanyia kazi ili kluondoa urasimu katika masuala ya ukadiriaji wa kodi.

"Tuna shida kubwa kwenye masuala ya ukadiriaji, ndiyo maana tuna mrundikano mkubwa sana wa kesi kwenye vyombo vyetu. Kwa hiyo Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa ukadiriaji, kuna shida moja tu na sisi kama serikali tumeliona.

"Moja ukadiriaji. Ile ya kwamba mimi ninakukadiria usiporidhika, kesho uje tuongee na mimi mwenyewe; na usiporidhika nenda kwenye hatua nyingine. Lakini ili usikilizwe huko unakokwenda ulipe kwanza theluthi moja ya kile ambacho umekikataa.

"Mheshimiwa Spika, hivi theluthi moja ya bilioni 150 ni ngapi? Theluthi moja ya bilioni 90 ni ngapi? Sasa tunapendekeza, tunapokwenda tutaanzisha chombo cha usuluhishi wa masuala ya kikodi.

"Tuwatengenezea watu wetu badala ya kutumia njia moja ya kupeleka malalamiko katika mahakama na kikodi pamoja na Bureau za Kikodi (mikoa ya kikodi).

"Tunataka wawe na sehemu ya kusemea mambo yao, lakini tunaendelea kuimarisha ile mifumo ya ndani ili pasiwe na uonevu kwenye ukadiriaji wa kodi," alisema.

Kutokana na malalamiko mengi, Waziri Mwigulu ameliriarifu Bunge kwamba serikali inataka mtu akadiriwe kodi anayostahili na kuanzia Julai Mosi mwaka huu, italifuatilia kwa karibu suala hilo.

Jana Bunge lilipitisha bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha ambayo imeongezeka kutoka Sh. trilioni 36.33 ilivyopendekezwa wakati wa uwasilishwaji wake hadi kufikia Sh. trilioni 36.68 baada ya kuongezwa fungu mahususi kwa sekta za afya, elimu na ujenzi (barabara).

## HABARI KITAIFA

# Tahadhari corona III yatolewa kila kona

**Na Mary Geofrey**

WAKATI serikali ikitoa tahadhari ya viashiria vya wimbi la tatu la ugonjwa wa Covid-19, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini (KCMC), zimeagiza wanaokwenda kupata huduma wavae barakoa na kutoa utaratibu mpya wa kuona wagonjwa.

Katika taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa MNH, Aminiel Aligaesha (pichani), utamaduni wa uvaaji barakoa, unawaji mikono na matumizi ya vitakasa mikono vitaendelezwa.

"Uongozi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili unatoa maelekezo kwa wagonjwa, wafanyakazi, wanafunzi na wananchi wote wanaoingia eneo la Upanga na Mloganzila kuzingatia kuvaa barakoa wawapo mazingira ya hospitali," alisema Aligaesha.

Pia alisema hakuna mfanyakazi au mwanafunzi atakayeruhusiwa kutoa huduma kwa mgonjwa bila kuvaa barakoa kuanzia kliniki, kwenye vipimo na wodini.

Kadhalika alishauri idadi ya wasindikizaji kwa wagonjwa wanaokwenda kliniki kupungua na mgonjwa ataruhusiwa mmoja tu.

"Wagonjwa waliolazwa wodini wataruhusiwa kuonwa na ndugu zao watano tu kwa siku ambapo asubuhi ni ndugu wawili, mchana mmoja na jioni wawili," alisema.



Aliwataka wananchi, kuunga mkono hatua hizo ili kuongeza tahadhari za kujikinga dhidi ya ugonjwa huu wa COVID-19 na kwamba hatua hizo zitaanza kuchukulia kuanzia leo.

Kwa upande wake, KCMC imetangaza utaratibu mpya wa kutumia ndugu mmoja kumuuguza mgonjwa katika kupunguza kasi ya maambukizi ya corona.

Taarifa iliyotolewa katika hospitali hiyo, ilieleza kuwa utaratibu huo, ulianza rasmi Juni 21 na ndugu atakayemuuguza mgonjwa atapatiwa kitambulisho maalum. Tangazo hilo liliwagusa pia wagonjwa wanaoenda kliniki kwenda peke yao na wale wasiyojiweza wataenda na ndugu mmoja.

Nacho Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), kimeainisha hatua madhubuti zinazopaswa kuchukuliwa ili kuepusha wimbi la tatu la kuingia na kusambaa kwa maambukizi ya virusi hivyo.

Rais wa MAT, Dk. Shedrack Mwaibambe, amenukuliwa na moja ya chombo cha habari, akitaja baadhi ya hatua zinazopaswa kufanywa kuwa ni kudhibiti idadi ya abiria katika vyombo vya usafiri na kuweka idadi ndogo ya mikusanyiko ya watu katika matukio.

Alifafanua kuwa kama ugonjwa upo, tahadhari zichukuliwe kwa kuunda sera au sheria ndogo kama vile kupunguza idadi ya watu katika matukio kama ya harusi.

Kwa mujibu wa MAT, wananchi wanapaswa kuwa makini kwa kuchukua tahadhari ikiwa ni pamoja na kuvaa barakoa, kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na kutumia vitakasa mikono.

# Mapya yaibuka 'house girl' anayedaiwa kunyonga mtoto

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

TUKIO la mtoto wa mwaka mmoja na nusu kudaiwa kunyongwa hadi kufa na msichana wa kazi limechukua sura mpya baada kuhusishwa na imani za kishirikina huku ikidaiwa kuwa ni tukio lake la tatu.

Wakizungumza jana na Nipashe kwa nyakati tofauti, majirani wa eneo la tukio walizungumzia mazingira ya mauaji hayo huku Mwenyekiti wa Mtaa wa Olkeriyani, Kata ya Olasiti jijini Arusha, Aminiel Mollel, akitoa tahadhari kwa waajiri kufahamu mazingira wanapotokea wasaidizi hao.

Mollel alisema alipata taarifa ya tukio hilo na kwenda kumchukua mtoto huyo hadi Hospitali ya Mount Meru, ambako baada ya uchunguzi waligundua ameshafariki dunia.

"Katika kumhoji msichana wa kazi alisema huyo ni mtoto wa tatu kumnyonga na wakati anamnyonga hakuwa na akili yake, lakini akishamaliza ndiyo inarudi, tunafikiri ni nguvu za giza zinamwendesha kufanya matukio haya," alisema mwenyekiti huyo.

"Watu walipofika nyumbani walimkuta anaosha vyombo kama hakuna kilichotokea," alisema.

Mwenyekiti huyo, aliwashauri wazazi na walezi kuwaajiri wasaidizi wanaojulikana mazingira waliyotokea ili kuwafahamu kabla ya kuwaleta majumbani mwao.

Mmoja wa majirani aliyejitambulisha kwa jina moja la Natalia alisema taarifa za kuuawa kwa mtoto huyo walizipata Juni 19, mwaka huu, majira ya saa 4: 00 asubuhi wakati mama wa mtoto alipokuwa ameshaenda kazini.

"Mama yake huwa amezoea kumwandalia kila kitu mwanawe, kabla ya kuondoka kwenda kazini anahakikisha amempikia na kumwogesha mtoto ndio amwachie binti huyu, na alikuwa akifanya hivyo kwa kuwa msichana alikuwa mdogo na pia alikuwa bado mgeni, tangu aje alikuwa na wiki mbili tu hapa," alisema Natalia.

Jirani mwingine ambaye alijitambulisha kwa jina moja la Rose, alisema mtoto wake aliitwa na msichana huyo wa kazi akimwambia kuwa haelewi kwanini mtoto haamki anapomuamsha jambo lililomfanya mtoto huyo akimbie kumuita.

"Nilikuja kumwona mtoto ikabidi nimwangalie joto la mwili lilikuwa bado lipo, lakini mtoto alikuwa hafanyi chochote nikambeba na kumtoa nje, tukaangalia tukaona shingoni kwekundu na kama kumenyofolewa nyofolewa," alisema na kuongeza;

"Nilimuuliza dada mtoto amefanyeje kwa haraka nilidhani labda zipu ya nguo imemuumiza, lakini alinyamaza huku akiendelea kuosha vyombo...ni tukio baya sana inauma sana," alisema jirani huyo.

Naye mama mkubwa wa marehemu aliyejitambulisha kwa jina la Judith, alidai baada ya binti huyo kumnyonga mtoto aliendelea na shughuli zake za kufua bila kujali tukio hilo.



# Mbunge CCM adai mshahara 'kiduchu'

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Mbogwe (CCM), Nicodemus Maganga, ameitaka serikali kuongeza maslahi ya wabunge zikiwamo posho na mishahara yao ili kuendana na mabunge mengine.

Amesema mabunge kama vile Afrika Kusini na Kenya wabunge wake wanalipwa mishahara na posho nzuri huku akidai maslahi ya sasa ya wabunge wa Bunge la Tanzania hayatoshelezi.

Mbunge huyo alitoa kauli hiyo bungeni juzi alipochangia makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema yapo manung'uniko ya aina hiyo miongoni mwa wabunge lakini wengi wao wamekuwa wakisita kuliweka wazi suala hilo kutokana na uoga.

Aliwashauri wabunge wenzake kutokuwaogopa wananchi katika suala la kudai maslahi yao na ikibidi kuwaambia ukweli wa hali ilivyo. Maganga alisema kuwa katika baadhi ya mabunge, wabunge wake wanalipwa posho na mishahara kwa dola, hivyo kuitaka serikali kuangalia upya suala hilo.

"Kuna manung'uniko kwa wabunge, maslahi ya wabunge Mheshimiwa Naibu Spika (Dk. Tulia Ackon aliyekuwa anaongoza kikao) kweli yapo kidogo sana.

"Wakati bado sijaingia humu nilikuwa ninafikiria kwamba kuna posho za kutosha. Nimeangalia mabunge mengine Afrika Kusini pamoja na Kenya na mabunge mengine wanalipa kwa dola. Tusiwaogope wananchi, lazima tuwe wakweli," alisema.

Maganga alisema wabunge wamekuwa wakitukanwa katika mitandao ya kijamii kwa mtazamo kwamba wanalipwa mishahara mikubwa, jambo alilodai halina ukweli wowote na hakuna kinachoendelea kwa wananchi wa majimbo yao kutokana na uhaba wa fedha.

"Tuwaambieni wananchi huku kwenye ubunge hakuna kitu, tumekuwa tukitukanwa kwenye mitandao, na mimi hii kazi niliomba kwa roho yangu moja na mimi nitasema ukweli daima, fitina kwangu mwiko.

"Pesa inayolipwa posho hapa (bungeni) haitoshi, mishahara haitoshi, mimi ninayeishi na wananchi, hakuna kinachoendelea.

"Kwa hiyo, hilo serikali iliangalie upya ili na sisi tufanane na mabunge mengine, tusiwe wajanjawajanja. Ninaujua utapeli wa kila aina lakini sitaki niwe tapeli kwa wananchi, wananchi wajue kwamba kuna mbunge mwenye hela kumbe hakuna kitu," alisema.

Mbali na mshahara, wabunge hulipwa posho wanapokuwa kwenye shughuli za Bunge zinazofikia Sh. 340,000 kwa siku na wakimaliza muda wao wa miaka mitano, hupata kiinua mgongo kisichokatwa kodi.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Prof. Mkumbukwa Mtambo (wapili kulia), akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkuu wa Uendeshaji wa Kampuni ya Plasco Ltd, Alimiya Osman, wakati alipotembelea kiwanda hicho, Chang'ombe, mkoani Dar es Salaam. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Plasco, Aunali Rajabali. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mabilioni yatengwa kishindo elimu bure

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imelazimika kuongeza bajeti ya Sh. bilioni 125 kwenye Sekta ya Elimu kwa ajili ya ujenzi wa maboma ya madarasa.

Nyongeza hiyo ya bajeti inalenga kukubaliana na idadi kubwa ya toleo la kwanza la wanafunzi wa mpango wa elimu bila malipo, maarufu elimu bure, ambao watahitimu darasa la saba mwaka huu na kujiunga na kidato cha kwanza mwakani.

Vilevile, serikali imetangaza kuongeza Sh. bilioni 70 katika bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kutoka Sh. bilioni 500 iliyokuwa imetengwa awali, ili kuwapa mikopo hiyo wanafunzi wote walioomba mwaka jana na mwaka huu na kuikosa.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alitangaza uamuzi huo wa serikali bungeni jana alipohitimisha mjadala wa siku saba za Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/22 na Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22.

"Kuanzia mwaka kesho (2022) tunaenda kupata toleo la kwanza la wale wanafunzi walioandikishwa kwa elimu bila malipo, hasa elimu ya msingi ambao wanamaliza darasa la saba, waanze kidato cha kwanza.

"Tusipojipanga kwenye miundombinu kuanzia sasa, takwimu zinaonyesha tutakuwa na uhitaji wa vyumba vya madarasa wa kiwango cha juu sana na hatutaweza kufanya kwa muda mfupi.

"Tumefanya suala la elimu liwe na kuviziana kwa sababu miundombinu haitoshi. Sisi kama wizara tunayoshughulika na mipango, tunaona hili jambo tunaweza, tusilimalize mara moja.

"Lakini ni vyema tukaanza kupanga haya mambo tunakokwenda. Tumeona lazima tushughulike na miundombinu. Tunapendekeza tuanze na maboma 10,000.

"Tunapendekeza tupeleke Sh. bilioni 125 kwenye upande wa maboma na hapa kila halmashauri itaondoka na maboma yasiyopungua 10 ili kila mmoja aweze kwenda nayo," alifafanua.

Kwa mujibu wa Dk. Mwigulu, serikali itatekeleza mkakati wake huo mwaka hadi mwaka.

Aprili mwaka huu, Nipashe ilichapisha ripoti maalum kuhusu hatari itakayoibuka mwakani ikiwa serikali haitachukua hatua mapema kukabiliana na ongezeko la wanafunzi katika toleo la kwanza la wahitimu wa darasa la saba wa elimu bure.

# Ajali ya barabarani ilivyoua watu tisa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MADEREVA wawili kati ya watatu wa magari yaliyopata ajali iliyotokea eneo la Oil Com Nane Nane, Barabara Kuu ya Morogoro Dar es Salaam juzi, ni miongoni mwa watu tisa waliofariki dunia kutokana na ajali hiyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Fortunatus Musilimu, alisema jana kuwa ajali hiyo ilitokea saa tano usiku.

Madereva waliofariki ni Adam Ramadhani Binde (24), mkazi wa jijini Dar es Saalam, aliyekuwa anaendesha Coaster (T 689 DUK) na Chawa Chali, dereva wa lori la Dangote aina ya Howo (T 658 DJZ).

"Chanzo cha ajali hiyo ni basi dogo la abiria aina ya Coaster kujaribu kulipita gari jingine aina ya Toyota Cresta lililokuwa mbele, lakini akakutana uso kwa uso na lori hilo," alisema.

Akasema katika ajali hiyo dereva wa gari la tatu aina ya Cresta (T 563 ASA) lililokuwa linaendeshwa na Emmanuel Sembuche (31), alinusurika, ingawa gari lake liliharibika.

Kamanda Muslimu alisema watu watano walifariki dunia papo hapo katika eneo la tukio na wanne wakafariki dunia wakati wakipatiwa matibabu hospitalini.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Kessy Ngalawa, alisema walipokea majeruhi 25 na miili saba, lakini idadi ya vifo iliongezeka kufikia tisa baada ya majeruhi wawili kupoteza maisha wakati wanapatiwa matibabu.

# Kihongosi bosi UVCCM

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMATI Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), imemteua Kenani Kihongosi kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana UVCCM.

Kihongosi anaziba nafasi iliyokuwa wazi baada ya Katibu Mkuu aliyekuwapo, Raymond Mwangwala, kuteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro.

Kabla ya uteuzi huo, Kihongosi aliteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Iramba akitokea Wilaya ya Arusha.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma, baada ya kumalizika kwa kikao hicho, Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema uteuzi huo umefanyika kwa mujibu wa Katiba ya CCM.

## HABARI KITAIFA



Diwani wa Viti Maalum Kata ya Makojo, Musoma Vijijini mkoani Mara, Tabu Machumu, akikagua maendeleo ya mradi wa maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria kwenda vijiji vya Makojo na Chitare juzi, ambao unatekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF). **NA MPIGAPICHA WETU**

# 14 waachiwa huru kugeuza wenye ulemavu ombaomba

**Na Kulwa Mzee**

WAFANYABIASHARA 14 waliokuwa wanashtakiwa kwa kusafirisha watu wenye ulemavu kutoka mikoa mbalimbali na kuwageuza ombaomba mitaani ili wajiingizie kipato wameachiwa huru.

Washtakiwa hao 14 wameachiwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Kassian Matembele.

Akiiwakilisha Jamhuri, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kesi ilikuwa inatajwa, lakini Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) aliwasilisha hati ya kuonyesha hana nia ya kuendelea na shauri hilo.

Hakimu Matembele alikubali maombi hayo na kuwaachia huru washtakiwa wote. Mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo Sadkiely Meta (71), alifariki dunia.

Washtakiwa walikuwa wanakabiliwa na mashtaka 41, yakiwamo ya kufanya biashara haramu ya kusafirisha binadamu kinyume cha sheria, kukwepa kodi na kuisababisha hasara ya Sh. milioni 31 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Meta na wenzake 14 walikuwa wanadaiwa kusafirisha watu wenye ulemavu 37, wakiwamo watoto wenye umri wa miaka saba na 11 kutoka mikoa ya Tabora, Shinyanga na kuwaleta Dar es Salaam kwa kuwageuza kuwa ombaomba mitaani kwa lengo la kujiingizia kipato.

Mbali na marehemu Meta, washtakiwa wengine ni Yusuph Mbuani (35), Joseph Magafu (20), Emmanuel Salu, Gogad Mayenga (18), Samson Akunahai (26), Husein John (18).

Wengine ni Zacharias Paul (18), Dotto Shigula (19), Petro Simon (21), Emmanuel Sahani (38), Joseph Mathias (20), Massanja Paul (21), Aminiel Sangu (21) na Emmanuel Lusinge (25), maarufu kama Salimu.

Katika shtaka la kwanza, Meta na wenzake wanadaiwa kati ya Agosti 2020 na Januari mosi 2021 katika jiji la Dar es Salaam, waliongoza genge la uhalifu kufanya biashara haramu ya kusafirisha binadamu.

Shtaka la pili, hadi 25 ambalo ni kufanya biashara haramu ya kusafirisha binadamu na kuwatumikisha wenye ulemavu, linalowakabili Meta na Mbuani, wanadaiwa kati ya Agosti 2020 na Januari mosi, 2021 katika eneo la Tandale Wilaya ya Kinondoni, wanadaiwa kumtumikisha mwenye ulemavu Rashid Shija.

# Aveva, wenzake kujitetea Juni 29

**Na Kulwa Mzee**

RAIS wa Klabu ya Simba, Evans Aveva na viongozi wenzake wawili wanaokabiliwa na mashtaka saba ikiwamo matumizi mabaya ya madaraka wanatarajia kuanza kujitetea Juni 29, mwaka huu.

Washtakiwa hao walipanda kizimbani jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, wakati kesi yao ilipokuja kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa.

Wakili wa Serikali Sylvia Mintato alidai kesi ilikuja kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa, Wakili anayeendesha kesi hiyo, Wankyo Simon ana udhuru anasafiri kwenda Dodoma kikazi.

Mintato aliomba kesi hiyo iahirishwe ipangwe tarehe ya karibu kwa ajili ya washtakiwa kuanza kujitetea.

Mahakama ilikubali kuahirisha kesi hiyo hadi Juni 29, mwaka huu kwa ajili ya washtakiwa kuanza kujitetea.

Washtakiwa wengine ni Makamu wake, Godfrey Nyange maarufu Kaburu na Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili, Zacharia Hansppope ambao walikutwa na kesi ya kujibu katika mashtaka saba na kuondolewa mashtaka ya utakatishaji fedha.

Katika mashtaka ya kwanza, Aveva na Kaburu wanadaiwa kula njama ya kutenda kosa la matumizi mabaya ya madaraka.

Aveva na Kaburu wanadaiwa kutumia vibaya madaraka yao kwa kuandaa fomu ya kuhamisha fedha Dola za Marekani 300,000 kutoka kwenye akaunti ya Simba iliyoko Benki ya CRDB Azikiwe kwenda kwenye akaunti binafsi ya Aveva iliyoko Benki ya Barclays.

Pia Aveva na Kaburu wanadaiwa kwa pamoja kughushi nyaraka iliyokuwa ikionyesha Simba inalipa mkopo wa Dola za Marekani 300,000 kwa Aveva kitu ambacho sio kweli.

Aveva katika Benki ya CRDB anadaiwa kutoa nyaraka ya uongo ikionyesha Simba wanalipa mkopo wa Dola za Marekani 300,000. Anadaiwa kuwa katika Benki ya Baclays Mikocheni alijipatia Dola za Marekani 187,817 wakati akijua zimetokana na kughushi.

Kaburu anadaiwa kumsaidia Aveva kujipatia Dola za Marekani 187,817 kutoka kwenye akaunti ya Simba wakiwa wanajua fedha hizo zimetokana na zao la kughushi. Aveva, Kaburu na Hans Poppe wanadaiwa kughushi hati ya malipo ya kibiashara wakionyesha kwamba nyasi bandia zilizonunuliwa na Simba zina thamani ya Dola za Marekani 40,577 huku wakijua kwamba siyo kweli.

Aveva anadaiwa kuwasilisha hati ya malipo ya kibiashara ya uongo kwa Levison Kasulwa kwa madhumuni ya kuonyesha kwamba Simba wamenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola za Marekani 40,577.


**Sanlam** Life Insurance

**NAFASI ZA KAZI-AFISA MAUZO (RESIDENT SALES EXECUTIVES)**

Sanlam Life Insurance(T) Ltd, kampuni inayoongoza nchini Tanzania katika utoaji wa huduma za bima za maisha (Life Insurance) inatangaza nafasi (40) za kazi za Maafisa Mauzo ambao ni wakazi wa miji ifuatayo: Morogoro, Ifakara, Dodoma, Iringa, Sumbawanga, Songea, Njombe, Manyara, Moshi, Rombo, Tanga, Mtwara, Lindi, Musoma, Bukoba,Geita,Kigoma,Kahama,Singida,Tabora,Katavi na Simiyu.Wakazi wa miji husika wanakaribishwa kutuma maombi yao.

**Sifa za mwombaji:**

- Cheti cha kidato cha nne au cha sita
- Cheti au stashahada au shadada ya bima,utawala wa biashara, masoko, mauzo au mafunzo mbadala.
- Cheti cha bima (COP) kinapendelewa
- Awe na ari ya kupata kipato kikubwa kwa kufanya mauzo mengi.
- Uzoefu wa kuuza huduma za bima au huduma za kifedha nyinginezo unahitajika.
- Utayari wa kutoa huduma kwa wateja popote pale walipo utazingatiwa.
- Awe na uzoefu na uwezo wa kufanya mauzo kwa kujitegemea kwa usimazi mdogo.
- Awe na uwezo wa kuzungumza na kuandika Kiswahili na Kiingeza fasaha.
- Awe na uwezo kufanya hesabu za kujumlisha kwa usahihi
- Awe na uwezo wa kushawishi na kujenga mahusiano
- Awe tayari kufanya kazi kwenye tawi lililopo mbali na makazi yake ikibidi.
- Awe na umri kuanzia miaka 35 kwenda juu.

Kama una sifa tajwa hapo juu , tuma maombi yako kupitia anuani tajwa hapo chini au lete kwa mkono ukibanisha mji ambao wewe ni mkazi na ungependa kufanya kazi huko. :

**Mkuu wa Utumishi na Utawala,**
**Sanlam Life Insurance (T) Ltd,**
**P.o box 22229**
**Mtaa wa Ohio,**
**Jengo la Amani Place Ghorofa ya 9,**
**Dar-es-Salaam.**

216321302

**Au piga simu namba (022-2127151-4) kwa maelezo zaidi.**
**Maombi yapokelewe kabla ya tarehe 03/07/2021**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Nguvu sasa iongezwe kutoa elimu ya corona

**SERIKALI** za Jamhuri ya Muungano na Zanzibar zimetoa tahadhari dhidi ya mlipuko mpya wa janga la corona, na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari kuhakikisha wanakuwa salama muda wote.

Nacho Chama cha Madaktari Tanzania (MAT) kimetaka serikali kuchukua hatua stahili kwa vitendo dhidi ya tishio la kuibuka kwa wimbi la tatu la corona.

Katika maeneo ya huduma za afya wananchi wanatakiwa kuvaa barakoa kwa lazima, huku baadhi wakipunguza idadi ya watu wanaotembelea wagonjwa na wanaokwenda kwa ajili ya kliniki kwenda wenyewe.

Hadi sasa hakuna takwimu zilizotolewa rasmi na serikali kuonyesha hali ya maambukizi na vifo, huku kukiwa na shinikizo la mashirika ya misaada ya kimataifa kutaka nchi kuweka wazi takwimu zake.

Hatua ya serikali kusema wazi kuna tishio la wimbi la tatu ni nzuri na sasa nguvu kubwa ielekezwe kwenye elimu kwa wananchi, kwa kuwa mtaani watu wanaendelea na maisha kama kawaida bila tahadhari yoyote dhidi ya corona.

Kwenye vyombo vya usafiri wa umma watu wanapanda kwa kujazana na hakuna uvaaji wa barakoa, huku kwenye masoko na maeneo ya mikusanyiko hakuna tahadhari zozote muhimu ikiwamo kunawa mikono.

Rais Samia Suluhu Hassan, aliunda kamati ya wataalamu ili kuishauri serikali, na ilishatoa taarifa yake na kupendekeza nchi kukubali chanjo, lakini iwe ni hiari.

Tayari Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, limesema limepokea ombi la Tanzania kuingizwa kwenye mpango wa chanjo za corona, ingawa Msemaji wa serikali alikaririwa akisema kuwa taarifa itatolewa baada ya Baraza la Mawaziri kujadili mapendekezo ya kamati.

Kwa upande wa Zanzibar, Rais Hussein Ali Mwinyi, alisema watapokea chanjo na itakuwa hiari, na sasa tahadhari imetolewa na Waziri wa Afya kwa kuwataka watu kujikinga.

Kwa ujumla ni muhimu serikali ikaweka wazi takwimu ili kuonyesha uhalisia wa ukubwa wa ugonjwa huu nchini na kuwalazimisha wananchi kuchukua tahadhari.

Rais Samia ameonyesha kwa mfano kwa kuvaa barakoa kila mkutano au aendako huku wanaohudhuria kikao au mkutano wako kuwa wamevaa, ni jambo linalopaswa kuigwa na sekta nyingine.

Mathalani, bungeni kuna mkusanyiko mkubwa na ingepaswa waonyeshe kwa mfano uvaaji wa barakoa, ili kuhamasisha wananchi kuvaa, na hilo kitafanikiwa zaidi kwa kuwa wawakilishi wa wananchi watatuma ujumbe moja kwa moja kuwa kuvaa barakoa ukiwa kwenye mikusanyiko ni muhimu.

Aidha, kasi ya kutoa elimu kwenye maeneo ya mikusanyiko kama minada, masoko, mikutano na vikao mbalimbali ingeongezeka ili kudhibiti kasi ya kusambaa kwa ugonjwa huo.


Wataalamu wanaeleza kuwa virusi hivyo hubadilika muundo kadiri siku zinavyosonga, na ndiyo maana India ilikumbwa na aina mpya ya kirusi hicho, huku Uganda ikiingia katika awamu ya pili.

Bila kusisitiza umuhimu wa kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni kama ilivyofanyika mwaka jana, baada ya serikali kutangaza uwapo wa virusi hivyo, wananchi wataendelea kuzembea na hali itakuwa mbaya zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ma-DC wapya kumbukeni kuinua mabega hakutakiwi

Na Sabato Kasika

**RAIS** Samia Suluhu ameendelea na uteuzi wa wasaidizi wake, huku safari ikiwa ni zamu ya mkeka wa wakuu wa wilaya, uliochanganya 'damu changa' ili nayo ichangie kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya taifa.

Katika hotuba alizotoa kwenye uteuzi wa viongozi mbalimbali amewahi kuwasisitiza wafanye kazi kwa ushirikiano na kutoa onyo kuwa hatosita kumuondoa kiongozi yeyote ambaye atainua mabega.

Anawakumbusha kuwa asiwepo kiongozi wa kwenda kinyume na kuanza kuinua mabega yake au kufanya mambo yake, bali kuwatumikia wananchi katika eneo lake la kazi ili kuharakisha maendeleo.

Kwa maana nyingine ni kwamba, alitaka kuwambusha kuwa cheo ni dhamana na uongozi ni utumishi, hivyo kiongozi asidhani kuwa cheo ni matokeo ya jitihada zake binafsi, hivyo anaweza kufanya lolote analotaka.

Si vibaya wakuu wapya wa wilaya walioteuliwa na kuapishwa juzi na wakuu wao wa mikoa, wakazingatia maelekezo hayo ya mkuu wa nchi ili walete matokeo chanya ya maendeleo katika maeneo yao ya kazi.

Mbunge wa Bumbuli mkoani Tanga, January Makamba, aliwahi kugusia suala cheo na kufafanua kuwa ni sawa na koti la kuazima ambalo mtu unakuwa na mbwembwe kubwa ukiwa umelivaa.

Lakini akasema, siku koti hilo linapochukuliwa, mvaaji anakosa mahali pa kuficha uso wake, hivyo akawataka viongozi vijana kuelewa kuwa madaraka au vyeo walivyobeba ni kama koti la kuazima.

Mwanasiasa huyo aliamua kutoa ushauri huo kwa kile alichobainisha kuwa ameona baadhi ya nyadhifa au vyeo wanavichukulia kwa namna ambayo imewaingia zaidi kichwani, mabega yamekuwa makubwa.

Anakumbusha kuwa kuna la kujifunza pale kijana mdogo, unangoja dereva mtu mzima azunguke amfungulie mlango wa gari, ambebee mizigo, na kwamba viongozi vijana wanaofanya hivyo, ni wazi kuna shida.

Katika kile ambacho Makamba anakiamini huenda kuna ujumbe kwamba moja ya sifa ya kiongozi bora ni utu na unyenyekevu, hilo ni wazi kwani kinyume chake ni kuinua mabega na kuwaona wengine wote hawafai.

Kwa kuwa wateule wanakwenda kutekeleza ilani ya CCM, basi wakumbuke pia ahadi za mwanachama hasa ile ya tano isemayo; 'cheo ni dhamana, sitatumia cheo changu wala cha mtu mwingine kwa faida yangu'.

Kimsingi, kiongozi anayezingatia ahadi hiyo, hawezi kuinua mabega yake na atakumbuka kuwa cheo ni sawa na koti la kuazima ambalo wakati wowote mwenye nalo anaweza kulichukua, hivyo jambo la muhimu ni kutumia umma.

Iwapo kiongozi atazingatia ahadi hiyo, atafanya kazi kwa kuigusa hata ahadi ya pili ambayo inasema; 'nitaitumikia nchi yangu na watu wake wote' ili kuharakisha maendeleo.

Sasa kwa kuwa rais ameshasema kwamba, kiongozi atakayeinua mabega ataondolewa kwenye nafasi yake, basi ni vyema kila aliyeteuliwa atimize wajibu wake inavyotakiwa, ili 'asisaidiwe kazi' au kutumbuliwa.

Aidha, kama kila kiongozi atatimiza wajibu wake inavyotakiwa, hakutakuwa na mtindo wa kujitwalia madaraka mikononi awapo kwenye kituo chake cha kazi, kwa kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na maelekezo ya rais.

Mtindo wa kujitwalia madaraka uliwahi kushamiri miaka ya nyuma hasa kwa baadhi ya wakuu wa wilaya kuweka watu ndani wanasiasa na watu wengine na kusababisha malalamiko. Pia kupora mali za wananchi.

Hatua hiyo ilimwibua aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Tawala za Mikoa (TAMISEMI), Seleman Jafo, kuingilia kati na kukemea mtindo huo wa kutumia vibaya madaraka kwa kuwaweka watu ndani.

Alikumbusha kuwa kuna sheria ya TAMISEMI ya mwaka 1997, kifungu cha 15 (1) inayowapa mamlaka wakuu wa mikoa na wilaya kutoa amri ya mtu kukamatwa na kuwekwa ndani kwa saa 48 anapobainika mhusika ametenda kosa fulani.

## Meya avutiwa upunguzaji msongamano shuleni Dar

**Na Beatrice Moses**

MEYA wa Jiji la Dar es Salaam, Omar Kumbilamoto, ameeleza kuvutiwa na juhudi za kuanzishwa kwa ujenzi wa Jengo la Taaluma kwenye Shule ya Msingi ya Olympio la ghorofa tatu, kwamba litapunguza msongamano wa wanafunzi na kuanzishwa rasmi kwa madarasa ya elimu ya awali.

Akizungumza jana kwenye hafla ya maombi maalum ya kuomba kuanza na kufanikiwa ujenzi huo, Meya Kumbilamoto aliahidi kuhamasisha baraza la madiwani kuona umuhimu wa halmashauri kuchangia kwa utaratibu uliopo.

Alisema shule hiyo ambayo kwenye matokeo ya mtihani wa Taifa wa darasa la saba ilishika nafasi ya kwanza Wilaya ya Ilala, ni miongoni mwa shule zinazoonyesha juhudi za wazi za kuleta maendeleo kwenye sekta ya elimu, hivyo inapaswa kuuongezewa nguvu ili kufanikisha ujenzi huo, hatua ambayo anaamini itasaidia katika kuwapa nafasi wanafunzi kufundishwa wakiwa wamepangwa kwa utaratibu utakaowawezesha kufanya vyema zaidi kwenye masomo.

Sheikh wa Wilaya ya Ilala, Shaban Mwinyipingu, aliongoza dua hiyo kwa upande wa Waislam wakati kwa Wakristo maombi yaliongozwa na Mchungaji Msaidizi wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) Kinondoni, Jacob Kassim, ambapo waliohudhuria waliipongeza hatua ya kamati ya shule na walimu kuona umuhimu wa kumtanguliza Mungu kwenye jambo hilo, hivyo litafanikiwa.

# Vigogo idara waonywa kuminya haki watumishi

**Na Mandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, amesema serikali haitomvumilia Mkuu wa Idara yeyote katika taasisi ya umma atakayesababisha mtumishi kukosa stahiki yake na mwananchi kukosa huduma bora.

Mchegerwa aliyasema hayo wakati akifungua kikao kazi cha mwaka cha Wakuu wa Idara za Utawala na Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma kilichofanyika Chuo cha Mipango jijini Dodoma jana.

Aliwataka wakuu hao kutekeleza majukumu yao kikamilifu ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kwa viongozi katika taasisi za umma kutenda haki kwa watumishi walio chini yao na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Aliwataka viongozi hao kutatua kero za watumishi na wananchi pindi wanapofuata huduma katika maeneo yao ya kazi na kuongeza kuwa pindi atakapofanya ziara katika maeneo yao hategemei kukuta foleni kubwa ya wananchi wakisubiri huduma pasipokuwa na sababu ya msingi.

"Mimi, naibu waziri wangu na watendaji wa ofisi yangu tukifanya ziara katika taasisi yako, hatutegemei kukuta mlolongo wa foleni ya wananchi wakisubiri huduma pasipo na matumaini yoyote," alionya.

Katika kutatua kero zinazowakabili watumishi na wananchi wanapohitaji huduma katika taasisi za umma, Mchengerwa ameanzisha mfumo wa kielektroniki unaoitwa 'Sema na Waziri Utumishi', ambao unatarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni ili kutoa fursa kwa watumishi na wananchi kuwasilisha malalamiko yao na kufanyiwa kazi.

"Kupitia mfumo huu, nitakuwa na uwezo wa kuona malalamiko yanayowasilishwa popote nitakapokuwa na kufanya ufuatiliaji wa namna yalivyofanyiwa kazi na ofisi yangu," alisema.


Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Festo Dugange, alisema Rais Samia amekuwa akisisitiza mara kwa mara matokeo chanya katika utekelezaji wa majukumu ya watumishi kwenye maeneo yao ya kazi.

Aliongeza kuwa ili matokeo hayo yaonekane, wakuu wa idara za utawala na rasilimaliwatu hawana budi kusimamia utekelezaji wa majukumu ya watumishi wa umma kwa ufanisi.

Kikao kazi hicho cha siku mbili kinahudhuriwa na wakurugenzi wa Idara za Utawala na Rasilimaliwatu kutoka kwenye wizara, idara zinazojitegemea, wakala, taasisi za umma, sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa.

## Lawyers without Boarders na vita dhidi ya Ujangili Afrika Mashariki

*Na Christina Mwakangale*




TAASISI ya Lawyers Without Borders (LWOB), imeendesha mashindano ya kushindanisha mawakili, kutoka nchi ya Tanzania na Kenya, kuwapata vinara wa uendeshaji mashtaka kuhusu haki za wanyamapori.

Katika mashindano hayo yaliyofanyika Mei mwaka huu, yalihusisha mawakili 24 kutoka nchi hizo, huku mawakili wanne wa Tanzania walioshiriki, waliibuka washindi.

Mwanasheria wa taasisi hiyo, Joseph Kisole alisema mashindano hayo yaliyofanyika kwa njia ya mtandao yalilenga kuwajengea uwezo mawakili wa kujitegemea na serikali, kutetea haki za wanyamapori.

"Lengo ni kubadilishana uzoefu wa kusimamia mashtaka ya wanyamapori namna ya kuendesha na kusimamia kesi mahakamani. Katika hilo mawakili walilofanya vizuri hutambuliwa," alisema Kisole.

Emmanuel Saghan, ambaye ni wakili alisema mashindano ni sehemu ya progaramu ya mafunzo yanayotolewa na taasisi hiyo, kuwaongezea ujuzi wa washiriki katika kazi zao za kisheria husus an kesi ngumu za uhalifu wa wanyamapori.

Alisema taasisi hiyo kupitia mashindano hayo yaitwayo, 'The Wildlife Crime (WICRI) Mock Trial' ni mpango wa miaka miwili unaofadhiliwa na Marekani.

"Mashindano ambayo yanafutia mafunzo kupitia uchambuzi wa kesi, utetezi na ushahidi namna ya uwasilishaji, ni muhimu kwa mawakili," alisema Saghan.

"Mafunzo katika programu hii yalibuniwa kimkakati, ili washiriki wanaofanya vizuri wanachaguliwa kuhudhuria programu za mafunzo mbalimbali kuwa mahiri namna ya kuendesha kesi hizo."

Saghan alisema kati ya mawakili 24 walioshiriki, mawakili wa serikali wanne kutoka Tanzania ikiwamo Chivanenda Luwongo, Meshack Lyabonga na Suzan Masule pamoja na wakili wa kujitegemea, Janeth Sekajingo, waliibuka washindi.

# UNDP, TADB watekeleza miradi 12 ya kuinua kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), wanashirikiana kutekeleza miradi 12 ya kuinua sekta ya kilimo. Utekelezaji huo utatumia njia za ubunifu badala ya kutumia utaratibu wa vigezo vya urari na ukwasi katika kufikira maombi ya mikopo na uwezeshwaji wa wakulima.

Jitihada hiyo ya pamoja kati ya taasisi hizo mbili imeelezwa jijini Arusha jana na Ofisa Miradi wa UNDP, Amon Manyama, wakati wa kikako cha pamoja baina ya wawekezaji kutoka Ulaya, viongozi wa serikali na taasisi za kimkakati za kuinua sekta ya kilimo.

Mkutano huo ulioitwa na Wawekezaji wa Ulaya katika Kilimo cha Tanzania (European Investors in Agricultural Dialogue), uliandaliwa na European Business Group nchini na umehudhuriwa pia na Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda na Balozi wa Uholanzi nchini, Jeroen Verheul.

Manyama hakueleza thamani ya miradi yote na mahali inakotekelezwa, lakini alisema utekelezaji huo unaongozwa makubaliano ya awali kati ya taasisi hizo mbili.

Akiunga mkono maelezo ya Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, aliyoyatoa kabla yake, Manyama alisema upelekaji fedha ya kuinua sekta ya kilimo katika nchi zinazoendelea kama Tanzania unadai ubunifu na umakini katika kupima maelezo na maombi ya mkopaji badala ya kutumia utaratibu unaotumiwa na benki ya biashara wa kupitia vigezo vya urari na ukwasi wa mwombaji. Amezitaka benki na serikali kutumia ubunifu katika kufikiria mahitaji ya fedha ya sekta ya kilimo.

"Ili kilimo kifanikiwe, unahitajika mtazamo mpya na tofauti na ule uliozoeleka katika kupeleka fedha katika sekta hii. Wakati taasisi za fedha zatazamiwa kufikiria namna tofauti ya kuhudumia kilimo, serikali pia lazima ichunguze fursa mpya za kupata fedha ya kupeleka katika kilimo.

"Kilimo, kama alivyoeleza Prof. Mkenda, kinaajiri zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania. Maana yake ni kwamba uwezo wa kilimo ukitumiwa kikamilifu malengo ya Ajenda 2030 yatafanikiwa bila wasiwasi. Nashauri serikali iangalie fursa mpya za kupata fedha na bidhaa za kifedha kwa ajili ya kilimo zikiwamo Blue Bond na Green Bond."

Justine aliueleza mkutano huo kwamba uelekezaji wa fedha katika sekta ya kilimo unahitaji majadiliano katika kufikiria maombi ya mikopo badala ya kutumia utaratibu wa kupitia vigezo vya urari na ukwasi wa mwombaji wa mkopo. "Ni kweli ili mchakato uwe na maana, lazima mradi unaoombewa mkopo uwe mzuri na stahiki. Lakini ni muhimu pia kuwa na majadiliano yenye sura ya ubunifu, kusikiliza na kupima kwa makini maelezo ya mwombaji mkopo," alieueleza mkutano huo.



Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifelo Sichwale (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Cornwell Tanzania, Elizabeth Lema, inayojihusisha na utengenezaji wa dawa za asili na virutubisho, wakati wa uzinduzi wa Klabu za Afya 'NMB Healthcare Club,' jijini Dar es Salaam jana. Wapili kushoto ni Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Makala ageukia deni la Machinga Complex

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, ameagiza uongozi wa Machinga Complex, Ilala, kufanya tathmini ya deni la soko hilo ili kuwekwe mikakati ya kulipa.

Aliyasema hayo jana alipofanya ziara ya kushtukiza katika soko hilo na kusema utaratibu wa ufanyaji biashara unaoendelea katika eneo hilo hakuridhishwa nao, hivyo kuagiza kuwekwe utaratibu utakaokuwa rafiki kwa wafanyabiashara wadogo na wakubwa.

Makala alisema jengo hilo limekuwa na mjadala wa muda mrefu, hivyo ni muhimu kuangalia ni namna gani litakuwa na tija hata kama fedha zilizokopwa haziwezi kurejeshwa kwa wakati.

Pia alisema kuna udhaifu wa viongozi kutokuweka utaratibu mzuri wa ufanyaji biashara ili wafanyabiashara wafaidike na serikali iingize mapato.

"Jengo hili lilijengwa kwa gharama kubwa lakini katika kumbukumbu hata deni mnalodaiwa hamlijui. Hawa NSSF waliotoa mkopo wako hapa hapa kwa nini deni msilijue. Naagiza mkurugenzi mkae mfanye tathmini tulijue deni kwani kutokulijua deni ndio maana mazingira hayaboreshwi," alisema.

Aliongeza kuwa diwani, mkurugenzi na katibu tawala wa eneo hilo wataweka utaratibu wa kwenda kusikiliza kero za wafanyabiashara na kuzitatua ili maendeleo ya eneo hilo yaonekane.

Serikali, alisema ina wajibu wa kuweka mazingira mazuri ya kuwafanya wafanyabiashara waendeshe shughuli zao katika eneo hilo. Pia alisema itaweka utaratibu wa kuondoa taka na kurekebisha miundombinu ya maji na umeme kuwa sawa.

"Kuna vichangamoto vidogo vidogo ambavyo vinahitaji uongozi wa karibu na wenye kauli na uhusiano mzuri na wafanyabiashara. Hata ng'ombe ukitaka kumkamua maziwa mpigie mlunzi kidogo atatoa maziwa lakini ukimpiga mateke na mijeledi lazima ataficha maziwa.

"Pia msifunge biashara za watu kwa sababu ya kodi. Wapeni muda wa kuongea, mtu unamdai fedha nyingi unamfungia biashara utazipataje hizo hela? Kuwapo na dawati tusitoe tu hukumu moja kwa moja muweke mikakati msipofanya hivyo na kukimbilia kufunga mtapoteza mapato," alisema.

# Kiini migogoro vyama wafanyakazi hiki hapa

**Na Mary Geofrey**

RAIS wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Tumaini Nyamhokya, amesema migogoro ndani ya shirikisho, vyama vya wafanyakazi na mabaraza inasababishwa na wajumbe waliowania nafasi za uongozi na kushindwa.

Ametoa rai kwa wagombea wa nafazi za uongozi kwenye vyama na mabaraza ya wafanyakazi, kukubali matokeo na kuendeleza umoja na mshikamano kwa uongozi uliopo madarakani kwa maslahi ya vyama.

Nyamhokya aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipofungua mkutano mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) wenye lengo la kufanya uchaguzi wa viongozi wa mkoa.

Alisema viongozi wanaokosa nafasi za uongozi hubaki na vinyongo vinavyosababisha makundi ndani ya vyama na baadaye kuzaa migogoro isiyomalizika.

"Ili kuwa na vyama vilivyo imara ni wajibu wa kila mwanachama anayewania nafasi ya uongozi kutambua kuwa kuna kushindwa ili ikitokea hivyo akubali matokeo na kubaki kuwa mwanachama mtiifu na siyo mwanachama mwenye magenge yake," alisema.

Nyamhokya alipongeza uongozi wa TALGWU na wanachama wake katika mikoa mitatu ya Ilala, Kinondoni na Temeke kwa kuwa waadilifu na kuwa miongoni mwa vyama vya wafanyakazi visivyo na migogoro.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu TALGWU, Rashid Mtima, aliwataka wanachama hao kufanya uchaguzi huru na haki.

Alisema mbali na kufanya uchaguzi, wanaangalia utendaji wa miaka mitano iliyopita na kuchambua ripoti za fedha na utekelezaji wake.

Alisema wanatarajia kuwa uchaguzi wenye tija ambao utazingatia mabadiliko ya miaka mitano ijayo kwa maslahi ya wafanyakazi.

HABARI KITAIFA

# Serikali yanena kuanzishwa kwa ‘Healthcare Club’

**Na Beatrice Moses**

BENKI ya NMB, imezindua Klabu za Afya ‘NMB Healthcare Club’, mtandao unaowapa wadau wa sekta ya afya, mikopo ya vifaa kazi, mitaji na uwekezaji, huduma inayokuja, huku serikali ikiipongeza.

Benki hiyo imetumia zaidi ya Sh. bilioni 32 kutoa mikopo kwa Sekta Binafsi ya Afya, kati ya Sh. bilioni 112.5 ilizopanga kutumia hadi mwaka 2025.

Klabu hiyo imezinduliwa sambamba na Kongamano la Afya ‘Tanzania Health Summit 2021,’ uzinduzi uliowakutanisha wadau wa Sekta ya Afya zaidi ya 150, wakiwamo madaktari, wamafasia, wamiliki wa hospitali, zahanati, vituo na vyuo mbalimbali vya afya na viongozi wa vyama washirika.

Uzinduzi huo ulifanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, ambako Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifelo Sichwale, aliyemwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, aliipongeza NMB kwa kuwaunganisha na kuwapa uwezeshaji wadau muhimu wa Sekta ya Afya.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Dk. Sichwale alibainisha kuwa wajibu wa kutoa huduma kwa wananchi, zikiwamo za afya ni wa serikali, lakini fursa na uwezo havitoshelezi, hivyo kufungua milango kwa sekta binafsi ya afya, na kwamba wataendelea kushirikiana na wadau wote wanaohudumu katika sekta hiyo.

“Uzinduzi huu unaofanyika leo una baraka zote za serikali na tunawaunga mkono kwa juhudi zenu za kuwaunganisha madaktari na wadau wengine muhimu wa sekta ya afya hapa nchini, katika kusapoti malengo ya serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuboresha mazingira ya sekta hii.

“Malengo ya Serikali ni kuboresha mazingira ya wafanyabiashara kushiriki kukuza uchumi wa Taifa kupitia kodi wanazolipa, kutoa ajira na kuongeza mitaji. Tunaamini kupitia NMB Healthcare Club, wanachama watapata mafunzo kuhusu maarifa ya kibiashara pamoja na elimu kifedha,” alisema Dk. Sichwale.

Naye Kaimu Ofisa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa benki hiyo, Benedicto Baragomwa, aliwapongeza wadau wa Sekta ya Afya kwa mapambano katika kipindi cha janga la COVID-19, na kwamba wao kama benki waliwaunga mkono wateja wao kwa kuwapa ahueni za kifedha na kubadili mfumo wa urejeshaji wa mikopo yao.

“Ukaribu wetu kwa wateja ulilenga kuwawezesha kuhimili changamoto zilizotokana na janga la Corona. Kwa sababu sisi NMB tumekuwa mstari wa mbele katika kusaidia sekta hii ya afya, ambako tunatoa misaada ya vifaa tiba, vikiwamo vinavyolenga kuhudumia eneo lenye changamoto nyingi, la afya ya uzazi.

“NMB tumeingia kwa nguvu moja kuhakikisha huduma bora za afya zinapatikana kwa wote, ambapo kupitia huduma ya Asset Financing - inayotoa mikopo nafuu mahsusi kwa Sekta Binafsi ya Afya, tumetumia zaidi ya Sh. bilioni 32 hadi Machi mwaka huu, kati ya Sh. bilioni 112.5 tulizopanga kutumia hadi mwaka 2025.

Kwa upande wake, Rais wa Tanzania Health Summit, ambaye ni Mkuu wa Idara ya Phisiolojia Chuo Kikuu Cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Dk. Omary Chillo, aliiomba serikali kuongeza nafasi za wadau wa sekta binafsi ya afya kushiriki vikao vya mipango kazi wizarani.

Naye Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Shedrack Mwaibambe, aliitaja NMB kama benki ambayo haijawahi kuacha kujaribu katika kila eneo kuhakikisha inaikwamua sekta ya afya Tanzania.

# Viwanda vya samaki hatarini kufungwa

**Na Richard Mkore,**
MWANZA

BAADHI ya wawekezaji katika viwanda vya kuchakata minofu ya samaki jijini Mwanza, wapo hatarini kufunga biashara zao, kutokana na kukosa malighafi za kutosha pamoja na samaki kupanda bei.

Wamesema baadhi yao imekuwa vigumu kufikia malengo waliyotarajia, ikiwamo kupata samaki wa kutosha, na kwamba soko la minofu ya samaki nje ya nchi ni kubwa na wanapata wateja wengi wanaohitaji, lakini samaki hawapatikani.

Satuh Poojery kutoka CMG GROUP, alisema wawekezaji wapo tayari kufanya kazi za uzalishaji kwa kiwango kikubwa, lakini baadhi yao wanakosa malighafi.

Alisema wavuvi wamekuwa wakiwauzia samaki kwa bei ya juu, na kwamba hatua hiyo inawafanya washindwe kushindana katika soko la nje.

Kwa upande wake, meneja wa kiwanda cha kuchakata minofu ya samaki cha Pesca Perch Ltd, Suresh Yonse, alisema wamemaliza ujenzi wa kiwanda, lakini upatikanaji wa malighafi umekuwa mgumu pamoja na bei kuwa juu.

Msemaji wa Chama cha Wavuvi Tanzania (TAFU), Sijaona Karoli, akizungumza kwenye kikao kati ya wawekezaji na Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), kilichofanyika jana jijini Mwanza, alisema tozo za kodi kwa wavuvi imekuwa chanzo cha kupanda bei ya samaki.

Aidha, alisema tozo hizo pia zinasababisha wavuvi kutorosha samaki nje ya nchi, badala ya kuziuza kihalali katika soko la ndani na kwa bei nafuu.

Aliongeza kuwa licha ya kuwapo uhaba wa samaki na bei kupanda, lakini pia wenye viwanda kwa asilimia 70 wanachelewesha malipo wanapopelekewa samaki na mawakala.

Karoli alisema tatizo lingine linalowakumba wavuvi ni kukosa fursa za mikopo kwa kuwa benki nyingi hazikubali kuwakopesha jambo ambalo linawafanya washindwe kukuza mitaji yao ili kuongeza shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria.

Aliongeza kuwa sheria ya uvuvi namba 22 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2020 zinawaumiza kwa tozo la asilimia mbili ya mapato yao.

Akizungumza katika kikao hicho cha wawekezaji, Meneja wa TIC, Kanda ya Ziwa, Pendo Gondwe, aliwataka kuwasaidia wajasiriamali wadogo ambao wanafanya nao biashara ili waweze kukuza mitaji yao.

Alisema TIC ipo tayari kukutana na wawekezaji wa aina zote katika kanda ya ziwa na maeneo mengine ili kusikiliza shida zao pamoja na kupokea ushauri.

Kuhusu tozo za kodi kwa wavuvi, alisema atahakikisha analifikisha suala hilo katika taasisi za serikali zinazohusika ili kuona namna bora ya kulitatua na kupata majibu ya kudumu kwa pande mbili.




Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo Tanzania, Simon Karikari (katikati), akichangia mada ya mjadala ulioandaliwa na kampuni hiyo kwa wadau mbalimbali zikiwamo tasisi za kibenki, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu teknolojia ya kidijitali kutoka kampuni za simu zinavyorahisisha mawasiliano na huduma kuwafikia wananchi licha ya kuwapo janga la COVID-19 tangu mwaka 2019. Kulia ni Mmiliki na Mwanzilishi wa kampuni ya Empower, Miranda Naiman na Mkuu wa Ubunifu na Mikakati wa Clouds Media Group, Reuben Ndege. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# KCB yaona fursa ajira kwa vijana

**Na Zuwena Shame**

MKUU wa Masoko na Masuala ya ushirikiano wa Benki ya KCB, Christina Manyenye, amewataka vijana kuchangamkia fursa za ufundi na ujasiriamali ili wajiajiri badala ya kukaa mtaani wakisubiri ajira.

Aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa mahafali ya kwanza ya wahitimu 163 katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) waliopewa udhamini na benki hiyo.

Manyenye alisema KCB iliwadhamini wahitimu hao katika fani za ujuzi, ufundi na ujasiriamali ikiwamo mapishi, ushonaji, ujenzi, ubunifu wa picha, upambaji, udereva na urembo.

Manyenye alitoa rai kwa vijana kukimbilia mafunzo ya ufundi stadi na ujuzi wa fani mbalimbali ili wajiajiri na kuondokana na dhana ya kusuburi ajira pindi wanapomaliza masomo yao.

“Ikiwa vijana wataona hizi fursa na kuziendea basi wanaweza kujiajiri na vilevile kuajiri vijana wenzao na hatimaye kuondokana na tatizo la ajira,” alisema.

Pia aliwataka vijana wasikate tamaa katika kutafuta maisha na watumia matatizo kuyageuza kuwa fursa na kufanya mambo mazuri.

Mkuu wa Kitengo cha Hazina, Pascal Machango, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, alisema KCB imeona fursa ya kuwezesha vijana kiuchumi kwa kuwapatia mafunzo na mitaji ya biashara.

Machango alisema kumekuwa na idadi kubwa ya watu lakini kwa upande wa ajira haziongezeki hivyo fursa ya pekee ni kujikita katika mafunzo ya ufundi stadi na ujarisimali ili vijana waweze kujiajiri.

Ofisa Utafiti na Mipango kutoka Baraza la Taifa la Uwezeshaji (NEC), Gwakisa Bwakala, alisema wameingia makubaliano na KCB na VETA kutoa mafunzo ya ujasiriamali, viwanda, ushauri na mikopo ambapo yanajumuisha wanafunzi kutoka Dar es salaam, Mwanza, Arusha , Kilimanjaro, Morogoro na Zanzibar.

Mkuu wa Chuo cha VETA, Joseph Mwanda, alisema katika ukuaji wa uchumi hakuna mapinduzi ya uchumi bila ujuzi kwa vijana.

Mwakilishi wa wahitimu hao, Mharami Nyambi, alisema mafunzo hayo yamewawezesha kutatua matatizo yaliyokuwa yakiwakabili husani tatizo la ajira na tayari miongoni mwao wamefungua biashara binafsi na kuajiri vijana wenzao.

HABARI BUNGENI

# Ndugai afunguka askari wenye tuhuma hifadhini

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema hatasita kuunda kamati ya kuchunguza tuhuma za matukio yanayofanywa na askari wa hifadhi kama Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro asipozungumza nao.

Ndugai alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu mwongozo uliioombwa na Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko. Katika mwongozo wake, mbunge huyo alitaka kujua ni kwa nini serikali isiunde kamati ya kuchunguza matukio ya kwenye hifadhi ambayo watumishi hao wanalalamikiwa.

Spika Ndugai akitoa majibu ya mwongozo huo, alisema askari wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) wamegeuka kuwa majangili badala ya kuwa msaada.

"Uzoefu unaonyesha kamati zikiundwa huwa haziwaachi salama hivyo Waziri afanye hivyo mapema, zamani hakukuwa na kelele nyingi kwa askari hao ukilinganisha na sasa, ambapo kila kona wanalaumiwa na kupigiwa kelele hivyo lazima watazamwe," alisema.

Awali, Waziri Ndumbaro aliwataka wabunge kushiriki kutoa elimu kwa wananchi wasiingie hifadhini na kwamba atatoa taarifa za askari wa TANAPA wanakwenda kinyume ili wachukuliwe hatua.

Alisema askari 61 wamefukuzwa kazi ambao wamekutwa na hatia.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum, Cecilia Paresso, alihoji kauli ya Serikali kuhusiana na baadhi ya askari wa TANAPA wanaolinda Hifadhi ya Msitu wa Marang unaopakana na Kata ya Buger wilayani Karatu kujichukulia sheria mkononi na kuwaua wananchi wanaoingia kwenye hifadhi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mary Masanja, alisema si kweli kwamba askari wanapokuwa kwenye maeneo ya hifadhi hujichukulia sheria mkononi na kuwaua wananchi wanaoingia kwenye hifadhi.

Hata hivyo, alisema wananchi wengi hujitokeza wakiwa na silaha za jadi zikiwamo fimbo,

mishale, mapanga na mikuki ili kuwadhuru askari wa hifadhi na kupinga ukamataji huo wa mifugo na kuchukua mifugo yao kwa kutumia nguvu.

Alisema yamefanyika matukio mengi ya askari kunyang'anywa silaha au mifugo iliyokamatwa hifadhini na wananchi ambapo husababisha kutokuelewana kati ya askari wa hifadhi na wananchi.

"Kati ya mwaka 2013 hadi 2020 jumla ya matukio saba yalitokea ambayo yalihusisha wananchi kuwashambulia askari wa hifadhi kuwajeruhi na wengine kupoteza maisha," alisema.

Aidha, alisema serikali kwa kushirikiana na wadau pamoja na wananchi wa maeneo hayo imeandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi ambapo kwa sasa hati zinaandaliwa na baada ya uhakiki wananchi watakabidhiwa hati zao.



Spika wa Bunge, Job Ndugai akiongoza kikao cha Bunge, wakati wa kupitisha bajeti kuu ya Serikali ya mwaka 2021/2022, bungeni jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Jengo la utawala Halmashauri Sumbawanga latengewa bil. 1/-

BUNGE limeelezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali imetenga Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Sumbawanga.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kwela (CCM), Deus Sangu. Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji ni lini serikali itakamilisha ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Halmashauri ya Sumbawanga katika Mji wa Laela baada ya agizo la serikali la kuhamisha makao makuu.

Akijibu, Dk. Dugange alisema Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ni miongoni mwa halmashauri 30 zilizohamia kwenye maeneo mapya ya utawala mwaka 2019.

"Ili kuwezesha halmashauri kutoa huduma bora kwa wananchi serikali imeweka mpango wa ujenzi wa jengo la utawala utakaogharimu Sh. bilioni 2.7," alisema.Aidha, alisema Mei 2021, serikali imeipatia Sumbawanga Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuanza ujenzi.

"Katika mwaka wa fedha 2021/22 serikali imetenga Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuendelea na ujenzi huo, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga imesaini mkataba wa ufundi na Chuo cha Sayansi Mbeya kwa ajili ya ujenzi ulioanza jana," alisema.

Alisema serikali itaendelea kutenga fedha za ukamilishaji wa jengo hilo.

Katika swali lake la nyongeza, Mbunge huyo alisema wafanyakazi katika Halmashauri hiyo wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana.




Habari zote na Augusta Njoji

## Mnada wa chai kufanyika Dar mwezi Desemba

SERIKALI inatarajia kufanya kwa mara ya kwanza mnada wa zao la chai utakaofanyika Dar es Salaam Desemba mwaka huu, ukiwa ni mkakati wa kuimarisha mfumo wa soko la zao hilo.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alitoa kauli hiyo alipokuwa jana bungeni akijibu swali la Mbunge wa Lupembe (CCM), Edwin Swalle.

Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali katika kukwamua zao la chai ambalo ni miongoni mwa mazao ya kimkakati yenye changamoto nyingi nchini.

Akijibu, Naibu Waziri Bashe alisema serikali inatambua umuhimu wa zao la chai kutokana na mchango wake katika pato la taifa, ajira kwa wadau wanaohusika katika mnyororo wa thamani wa zao na kipato kwa wakulima wa chai.

"Katika kuongeza uzalishaji na tija ya zao la chai, serikali inaendelea kuwekeza katika utafiti na uzalishaji wa miche bora ya chai ambapo hadi kufikia Mei, 2021, Taasisi ya Utafiti wa zao la Chai Tanzania (TRIT) imezalisha aina mpya nane za zao la chai zinazohimili ukame, ukinzani na magonjwa, zenye tija nzuri ya uzalishaji na ubora wa vionjo vya kimataifa," alisema.

Hata hivyo, alisema Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) na TRIT kwa kushirikiana na Kampuni ya Mbolea ya Minjingu inaendelea na majaribio ya mbolea ya minjingu kwenye mashamba ya chai.

"Hatua nyingine ni kutoa mafunzo ya vitendo kwa wakulima 2,000 wa chai kupitia mashamba darasa 97 katika halmashauri za Wilaya za Njombe, Rungwe na Mufindi kwa lengo la kuongeza tija, ubora na ushindani wa chai ya Tanzania kwenye masoko ya kimataifa," alisema.

Hata hivyo, alisema katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, serikali imeendelea kuhamasisha wakulima wa chai kutumia umwagiliaji na baadhi ya wakulima chini ya makampuni ya Uniliver na DL wameanza kufanya majaribio ya matumizi ya mifumo ya umwagiliaji kwenye kukuza chai.

"Pia kupitia Mradi wa Agri-connect Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa ajili ya kuendeleza mnyororo wa thamani wa mazao ya chai, kahawa na bustani (mboga, matunda na viungo) katika mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Iringa, Songwe, Njombe na Katavi, barabara zilizojengwa hadi kufikia Mei, 2021 zina urefu wa kilometa 87.6," alisema.

Bashe alisema Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA) inaendelea kuhamasisha Vyama vya Ushirika katika zao la chai kutumia mfumo wa uagizaji wa mbolea kwa pamoja (BPS) ambapo Februari, 2021 Chama cha Ushirika wa mazao na masoko (Mkonge AMCOS) kilifanikiwa kuagiza tani 500 mbolea aina ya NPK kwa ajili ya zao la chai kupitia mfumo wa BPS kwa niaba ya vyama vilivyo wanachama wake.

"Serikali inaendelea kuimarisha mfumo wa masoko ya chai na ifikapo Desemba, 2021 tutakuwa na mnada wa chai nchini kwa mara ya kwanza ambao utafanyika jijini Dar es Salaam na kutoa fursa kwa wazalishaji wakubwa na wadogo kushiriki kwenye uuzaji wa chai ndani ya nchi badala ya kupeleka chai kwenye mnada wa Mombasa nchini Kenya," alisema.

Tanzania inavyoelekea kutinga 50/50

Ukurasa 12





Ukurasa 13

Chongolo anapotangaza mambo mapya CCM



Ukurasa 14

KENETH KAUNDA

Aliheshimu demokrasia ya vyama vingi, lakini...

siasa

JUMATANO JUNI 23, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# Ndilo balaa kubinya nafasi ya kiraia

• Raia kubambikwa kesi, kupanda umaskini

**Na Mwandishi Wetu**

MIAKA ya karibuni imeshuhudia jinsi kubinywa uhuru wa kutoa maoni na kubanwa nafasi ya kiraia (civic space) kulivyosababisha raia wengi kuumia baada ya baadhi ya 'vigogo' kuutumia mwanya huo kukandamiza watu.

Baadhi ya mambo yanayosababisha kubinywa eneo au nafasi ya kiraia ni kama kukosekana uhuru wa maoni, asasi za kiraia kudhibitiwa, kubana vyombo vya habari binafsi, kutunga sheria kandamizi, kukabwa koo taasisi za kidini, watetezi wa haki za binadamu na kudhibiti mitandao ya kijamii.

Kwa ujumla eneo au nafasi ya kirai ni uwanja ambao wananchi huutumia kuhoji, kudai haki zao, kukosoa serikali na taasisi nyingine za dola.

Kubinywa kwa nafasi hiyo ya kiraia miaka ya hivi karibuni kulisababisha wajanja kuwaumiza raia na kama ambavyo baadhi ya watetezi wa haki za binadamu wanavyosema.

Mwenyekiti wa Kamati wa Kitaifa ya Maaskofu na Mashekhe ya Maadili , Amani na Haki za Bindamu kwa Madhehebu ya Dini, Askofu William Mwamalanga, anasema baadhi ya wajanja walitumia sheria kuumiza wafanyabiashara na kuwaongezea Watanzania umaskini.

Aidha, anasema sheria hizo 'kandamizi', zimepunguza haki nyingi za Watanzania, akikumbusha kuwa baadhi zimetumiwa kukiuka utawala wa sheria, haki za binadamu na kuukandamiza uhuru wa kujieleza, kutoa maoni na kujitetea, kwa vile wengi hawakusikilizwa.

Anaisihi na kuipongeza awamu ya sita kwa kustawisha haki kwa Watanzania baada ya Rais Samia Suluhu, kuonya kuhusu kodi za dhuluma na mali za wafanyabiashara pamoja na kuwabambikia kesi za kuhujumu uchumi au za rushwa hakukubaliki.



Waziri wa Sheria na Katiba Profesa Palagamba Kabudi. **PICHA: MTANDAO**

Anasema uamuzi wa serikali kurejesha akaunti za wafanyabiashara zilizokuwa zimefungiwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuzungumzia utaratibu wa kurudisha fedha za washtakiwa zilizokuwa zimechukuliwa baada ya makubaliano na kukiri makosa kwa DPP.

Anasema kutumia sheria vibaya ambazo ni kandamizi ni kuvunja haki za binadamu na kushauri kuzifuta kwa vile zinahujumu maisha ya watu na kunyang'anya mali kwa kisingizio cha sheria.

Anagusia sheria za uhujumu uchumi na utakatishaji wa fedha akisema zimesababisha kubambikiza watu kesi, kufunga biashara zao na kuchukua fedha zao.

Anaonya kuwa matumizi hayo mabaya ya sheria hizo hivi karibuni yaliwanyima baadhi ya wananchi haki ya kumiliki fedha, kuwa na vitega uchumi na kumiliki akaunti zenye pesa nyingi benki.

Askofu huyo anakumbusha kuwa akaunti hizo zilikaguliwa, kufungiwa, fedha kuchukuliwa kinyume na sheria za kibenki na za nchi na kuwa chanzo cha umasikini kwa baadhi ya Watanzania.

"Vitendo vya kubambikizia kesi za utakatishaji fedha na uhujumu uchumi vimeumiza watu na hata kuleta chuki kwenye jamii hivyo kuna haja ya kuangalia tena sheria hizo," anashauri Mwamalanga.

### UHURU WA KUABUDU

Suala mojawapo linaloweza kuongeza nafasi za kiraia na kutoa maoni ni uhuru wa kuabudu ambao kiongozi huyu wa dini anasema nao ulianza kulalamikiwa kuwa kuna hofu ya kuuminya.

Anataja kuwapo urasimu kwenye usajili wa taasisi za dini akieleza kuwa kazi hiyo inaweza kufanyika kwa miaka mingi jambo ambalo linatazamwa kama kuuminya uhuru wa kuabudu ambao upo kikatiba.

Anaishauri serikali kuunda chombo cha kusajili taasisi za kidini pekee kama ilivyo kwa Msajili wa vyama vya siasa, kuepusha uwezekano wa kuwanyima watu uhuru wa kuabudu.

"Ibara ya 19(1) ya katiba ya Tanzania inampa kila mtu stahili ya kuwa na uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini, pamoja na uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake vile apendavyo hivyo inaeleza kuwa kila mwananchi anayo haki ya uhuru wa kuamini dini anayoitaka."

### MAHAKAMA YA AFRIKA

Sakata la Tanzania kukataza asasi za kiraia na hata watu binafsi kufikisha kesi kwenye Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na za Watu linatajwa kubana uhuru wa raia kutoa maoni na kudai haki.

Licha ya kwamba inasisitiza kuwa haijajitoa ukweli ni kwamba wananchi wake hawawezi kunufaika na uwapo wa chombo hicho kwani hawakitumii kudai haki zao.

Akizungumzia suala hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Anna Henga, anasema wakati umefika kuharakisha hatua ya kutengua uamuzi ya kujiondoa kwenye kipengele hicho.

Anakumbusha kuwa serikali ilishiriki mchakato wa kuanzisha mahakama hiyo iliyoko Arusha na ilikubaliana kuhusu utetezi wa haki za binadamu katika nchi za Afrika, pengine hakuna sababu ya kukataza mtu binafsi na asasi za kiraia wasishitaki.

"Tanzania imesaini na kuridhia na ilikuwa pamoja na viongozi wa Afrika, ikakaa na kukubaliana kuwa tunataka kuwa na chombo cha haki cha Afrika kwanini raia wake wabanwe?" anahoji.

Anakumbusha kuwa dunia ya leo inazungumzia na kusisitiza haki za binadamu na utawala wa sheria ikiwamo haki za Watanzania na mstakabali ni haki za Waafrika na hiyo ni demokrasia inayosimamia misingi wa sheria, katiba, haki za binadamu, na utawala bora, tunajiuliza kwanini Tanzania ijiweke pembeni?

Henga anasema kuna mambo mengi yanayotatiza demokrasia ikiwamo sheria ya kinga za viongozi ambayo inawapa viongozi mamlaka ya kufanya wapendavyo na baadhi huvunja katiba.

Haki ya kuwa na maoni ni miongoni mwa mambo ambayo yanakuza demokrasia na inapotumiwa kikamilifu ni kioo cha kujitazama kwa wanasiasa na mihimili mingine ya dola pamoja na sekta binafsi.

Yote hayo yanawezekana iwapo kuna utawala wa sheria unaoheshimu katiba na unaowapa wananchi haki za msingi ikiwamo kuwa na uhuru mpana wa nafasi ya kiraia.

Mwanafunzi wa Shule ya Sheria Dar es Salaam, Ruth Pallangyo, anakumbusha kuwa uwepo wa nafasi kubwa ya kiraia kutoa maoni, kujiunga na vyama wanavyovitaka, kujadili mambo yao iwe kwenye mitandao na mikutano ya hadhara na kukosoa pale wanapoona inafaa ni njia mojawapo ya kudumisha ustawi wa watu wanaojiamini. Pia huondoa chuki na hofu miongoni mwa raia.



Rais Samia Suluhu Hassan, pamoja na kinamama wafanyabiashara. Hivi karibuni ametangaza nia ya kushirikisha wanawake zaidi katika uongozi wa taifa. **PICHA: MTANDAO**

# Tanzania inavyoelekea kutinga usawa 50/50

**Na Christina Mwakangale**

IDADI ya wabunge wanawake Tanzania ni 143 baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka jana, ikiwa imeongezeka ikilinganishwa na kiwango chao kwa mwaka 2015.

Rais Samia Suluhu Hassan, anayasema hayo wakati akizungumza na wanawake mkoani Dodoma na kueleza kuwa mwaka 2015 walikuwa 127, idadi hiyo ikijumuisha wanawake kutoka majimboni, waliteule wa Rais pamoja na viti maalumu.

Kwa upande wa wanaharakati na watetezi wa haki za kinamama, wanaona kuwa wanawake wanaochaguliwa kwenye uwakilishi ni wachache mno, kwa vile idadi yao kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni asilimia 10.

Hayo yamo kwenye Ripoti ya Haki za Binadamu ya mwaka 2020, iliyoandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ikibainisha masuala kadhaa ya kijamii, kisiasa, kiuchumi kwa kipindi cha mwaka jana.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi, inaeleza kuwa Tanzania ina majimbo ya uchaguzi 264, Bara ikiwa na 214 wakati Zanzibar yako 50, kiwango cha asilimia kumi kinachotajwa na HLRC kinamaanisha kuwa wanawake waliochaguliwa na wapigakura ni 26.

Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga, akizungumza na Nipashe kutoa ufafanuzi zaidi, anasema malengo ya mikataba ya kimataifa kuhusu usawa wa kijinsia katika uongozi yanaweza yasifikiwe iwapo mabadiliko hayatofanyika kwenye eneo la kuwashirikisha kikamilifu wanawake.

> “ Nina imani kubwa wanawake wanaweza sana kuleta mabadiliko chanya katika vyombo vya maamuzi wakiwezeshwa na wakijiwezesha.

Upo mkataba wa kimataifa wa haki za wanawake za kwenye siasa wa mwaka 1952 na ule kutokomeza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake (CEDAW) wa mwaka 1979. Mikataba hiyo ambayo inaweka kiwango cha uwakilishi wanawake kufikia asilimia 50 kutoka 30, kwenye uongozi.

Henga akifafanua suala hilo na kuichambua ripoti hiyo, anasema ni wakati wa Tanzania kuchukua hatua zaidi kuongeza idadi ya wanawake katika ngazi za uamuzi.

Jitihada zimeanza kuonekana baada ya Rais Samia kuteua wanawake wengi kwenye ngazi za uamuzi ikiwamo kuongeza idadi ya wanawake kwenye maeneo ya utendaji mfano, Katibu wa Bunge, makatibu tawala wa mikoa, mawaziri akiwa wa Mambo ya Nje ambayo ni wizara nyeti.

Katika mkutano wa Rais Samia na kinamama mkoani Dodoma hivi karibuni anakumbusha kuwa uteuzi unaofuata utazingatia ajenda ya uwakilishi wa 50/50 kwa ngazi mbalimbali.

Rais anaahidi kuwa moja ya mikakati ya uongozi wake ni kufikia uongozi wenye uwiano wa kijinsia na unaoshirikisha wanawake.

### WABUNGE ASILIMIA 10

Henga akifafanua suala la idadi ndogo ya wabunge wa kuchaguliwa anasema kushinda viti vya ubunge kwa kuchaguliwa majimboni linatia wasiwasi, ikizingatiwa kuwa Tanzania ina wajibu katika mikataba na matamko mbalimbali ya kimataifa.

Henga anasema kati ya mikataba hiyo iliyoridhiwa na nchi ni pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SGDs), mkataba wa nyongeza kwenye mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake barani Afrika (Mkataba wa Maputo) wa mwaka 2003.

Pia, anasema ibara ya tisa ya Mkataba wa Maputo inatoa haki ya wanawake kushiriki katika mchakato wa kisiasa na kufanya maamuzi.

“Ibara hii inayataka mataifa, ikiwamo Tanzania, kuchukua hatua chanya mahsusi za kukuza utawala shirikishi na ushiriki sawa wa wanawake na wanaume katika maisha ya kisiasa ya nchi zao kupitia hatua za upendeleo maalum, sheria wezeshi na hatua nyingine za kuhakikisha wanashiriki katika uchaguzi bila ubaguzi.

“Ibara inabainisha kwamba uwepo uwakilishi sawa wa wanawake na wanaume katika ngazi zote na michakato yenye usawa ya uchaguzi.”

Henga anasema, ibara hii inayataka mataifa wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) kuhakikisha kunakuwapo na kuongezeka uwakilishi na ushiriki madhubuti wa wanawake katika ngazi zote za uamuzi.

### MAONI YA WACHAMBUZI

Mchambuzi wa masuala ya kisiasa, Abbas Atiki, anasema kwenye tafsiri halisi ya hatua maalumu zisizo za kudumu (temporary special measures) na ukomo wa ubunge ni vyema kuwekwa sawa na kubainisha ukomo wa viti maalumu kama ni miaka mitano, 10, 15 au 20.

Atiki anasema mara kadhaa imeshuhudiwa katika nafasi za ubunge wa viti maalum katika vyama vya siasa, wanaopata nafasi mara nyingi hujirudia na wengine hufikia hatua ya kustaafu siasa wakikalia viti hivyo baada ya miaka 10 au 15.

“Ninadhani kwamba labda kwa mujibu wa ibara hii ya CEDAW huenda ukomo ungekuwepo baada ya mbunge kuhudumu vipindi walau viwili kwani anaweza kuwa amewezeshwa kifursa, kiuchumi, kiutendaji na kiuamuzi bila ya kuathiri uwezo wake kiweledi,”

Pia anasema hiyo haimaanishi ama halizuii hatua zisizo za kudumu kwa zaidi ya vipindi viwili hasa kutegemea na uwiano baina ya wanawake na wanaume katika vyama vya siasa.

“Nina imani kubwa wanawake wanaweza sana kuleta mabadiliko chanya katika vyombo vya maamuzi wakiwezeshwa na wakijiwezesha.

“Rais Samia ni mfano wa namna wanawake na kina mama wanavyoweza kuleta matokeo chanya na makubwa katika nchi,” anasema na kushauri kujengwa mifumo imara ya kuwapata wanawake watakaovaa viatu vya wale watakaomaliza muda wao kisheria na kwa mujibu wa katiba.

# Chongolo anapotangaza mapya CCM

Na Mashaka Mgeta, TANGA

## • Moto wa chama sasa ni kuanzia mashinani



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo (aliyevaa skafu) akiwa Mkata maeneo aliyotembelea mkoani Tanga hivi karibuni. **PICHA: MASHAKA MUGETA**

BAADHI ya wanachama na wafuasi wa CCM mkoani Tanga, wanakitazama chama chao katika taswira mpya ya ushindani wa kisiasa, ikiwa ni takribani mwezi mmoja na nusu, tangu kuteuliwa kwa Katibu Mkuu Daniel Chongolo.

Chongolo aliingia katika uongozi wa chama hicho Aprili 30, mwaka huu, akichukua nafasi ya mtangulizi wake, Dk Bashiru Ali, ambaye hivi sasa ni mbunge wa kuteuliwa na Rais.

Akiwa katika ziara yake ya kwanza ya kikazi tangu kuteuliwa kushika wadhifa huo, Chongolo anawasili mkoani Tanga akiwa na ujumbe mahususi wa kukiimarisha chama hicho katika ngazi ya mashina.

Ujumbe wa Katibu Mkuu huyo unawajumuisha pia Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamidu Shaka na Katibu wa NEC-Siasa na Ushirikiano wa Kimataifa, Ngemela Lubinga.

Chongolo, amekuwa Katibu Mkuu wa 11 wa CCM tangu chama hicho kilipoanzishwa Februari, 5, 1977.

Makatibu wakuu na kipindi walichohudumu kwenye mabano ni Pius Msekwa (1977-1980), Daudi Mwakawago (1980-1982), Rashidi Kawawa (1982- 1990), Horace Kolimba (1990-1995), Lawrance Gama (1995-1997), Philip Mangula (1997-2007), Yussuf Makamba (20072011), Wilson Mukama (2011- 2012), Abdulrahman Kinana (2012-2018) na Dk.Bashiru Ally (2018-2021)

Katika ziara ya siku nne mkoani Tanga, Chongolo alitembelea wilaya za Kilindi, Handeni na Korogwe wakati Shaka alikwenda Pangani na Tanga Mji huku Lubinga akizuru wilaya za Lushoto na Mkinga na majumuisho ya ziara hiyo yakifanyikia Korogwe.

Chongolo anasema azma ya kukiimarisha chama hicho katika ngazi ya mashina inatokana na hitaji la katiba ya chama hicho, inayoelezea kuwa msingi wa uhai wa CCM unajikita katika ngazi hiyo ya chini kabisa kwenye jamii.

Chongolo anasema, ili kuhakikisha kila mwanachama wa CCM anashiriki shughuli za kwenye shina, miongoni mwa vigezo vitakavyotumika katika fursa mbalimbali ikiwamo nafasi za kuwania uongozi na uwakilishi wa wananchi, itakuwa ni rekodi ya ushiriki katika ngazi hiyo.

### ANATOA ONYO

Katibu Mkuu huyo wa CCM anasema kwa muda mrefu sasa, baadhi ya wanachama na viongozi wameyasahau mashina, badala ya kujielekeza katika mambo yasiyokuwa na tija kwa chama hicho, ikiwemo kupanga safu za viongozi, wabunge na madiwani.

"Kuna baadhi ya maeneo ambapo wana-CCM wananyoosheana vidole kwa kupanga safu za viongozi na wagombea wao, hivyo kuchangia upatikanaji wa viongozi wasiokuwa na sifa," anasema.

Kwa mujibu wa Chongolo, viongozi bora kwa maslahi ya nchi na watu wake huwa 'hawatengenezwi' kupitia safu zinazopangwa na wanasiasa na watu wenye maslahi binafsi, bali ni yule anayeibuliwa huku akitambua kwamba uongozi ni mzigo.

"Kuingia madarakani ni hatua nzuri kwa chama cha siasa, ingawa si jambo la kukimbilia... ni mateso kwa mtu anayepewa dhamana ya uongozi. Binafsi sikuwahi kufikiria ama kushawishi kupata nafasi hii...madaraka hayakimbiliwi, "anasema.

Anasema, viongozi 'wanaotengenezwa' ama kuyakimbilia madaraka hawana sifa, badala yake wamekuwa chanzo cha migogoro na mambo yasiyo na tija katika jamii, ikiwemo kuwapa wananchi matumaini hewa yanayotegemea miujiza badala ya kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo.

Chongolo anasema kutokana na dhamira na utashi wa kisiasa unaolenga kukiimarisha chama hicho kwenye ngazi ya mashina, ni marufuku kwa mwana-CCM yeyote kujihusisha na njama za kukimbilia uongozi, iwe ni kwa Uchaguzi Mkuu wa 2025 ama uchaguzi wa ndani ya chama hicho utakaofanyika mwakani.

### KUFUATILIA MIRADI

Katibu Mkuu Chongolo anasema kutokana na CCM kuwa katika uongozi wa nchi kupitia Ilani yake ya Uchaguzi Mkuu 2020, ipo haja kwa viongozi wake kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayofanyika kwenye maeneo yao.

Anasema kuna wakati ambapo serikali inalazimika kugharimia kazi zinazofanywa na 'vyombo'vyake kama Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kushughulikia upotevu wa fedha ambazo zingeokolewa kama ufuatiliaji ungefanyika kwa wakati husika.

### KUEPUKA MIFARAKANO

Chongolo anawaasa viongozi wa CCM na serikali katika ngazi tofauti kujikita katika kushughulikia kero za wananchi, huku wakiimarisha uhusiano na ushirikiano miongoni mwao.

"Hatuwezi kuwa na viongozi wa chama (CCM) na serikali wasioshirikiana ama kulewana, kwa maana hali hiyo inarudisha nyuma maendeleo ya nchi na watu wake...hali kama hii haivumiliki," anasema.

### HANDENI IGAWANYWE

Akichangia hoja katika ziara ya Chongolo, Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Handeni, Athuman Malunda, anasema miongoni mwa hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi, ni pamoja na kuigawa wilaya hiyo ki-chama, na kuzifanya kuwa mbili.

Anasema Handeni ina eneo la ukubwa wa takribani kilomita za mradi 7,800, hivyo kuwa kikwazo kwa viongozi wa CCM kuyafikia maeneo yote kwa wakati unaofaa, hoja ambayo Chongolo akaahidi kuichukua kwa ufuatiliaji.

### KUELEKEA 2025

Katibu Mwenezi wa CCM mkoa wa Tanga, Saida Mahugu, anasema ili kuyawezesha mashina ya CCM kujiimarisha na kuongeza wanachama zaidi, umepitishwa mkakati wa kuwashirikisha madiwani wanaotokana na chama hicho, kuwezesha upatikanaji wa kadi utakatumika pia kama sehemu ya chanzo cha mapato endelevu.

"Tukipata kadi 180 kwa kila kata na kuongeza zaidi idadi ya wanachama, ni wazi kwamba vikao vya mashinani vitakuwa na hoja zenye mashiko zitakazowatoa watu kwenye majungu, na badala yake kushiriki mikakati na mipango itakayotuingiza kwenye uchaguzi mkuu wa 2025 tukiwa imara zaidi," anasema.

### TAARIFA ZA FEDHA

Barnabas Essau ni Katibu wa CCM mkoa wa Tanga, anasema miongoni mwa kazi zinazopaswa kufanywa na viongozi wa chama hicho kwenye ngazi za msingi, ni kuhimiza watendaji wa vijiji na mitaa kuwasomea wananchi taarifa za mapato na matumizi kwa wakati.

Pia Essau anasema hivi sasa viongozi wa CCM mkoani humo, wanapaswa kusahau tofauti zilizojitokeza wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu wa 2020, badala yake kuelekeza nguvu katika umoja na mshikamano.

> Tunapojipanga kwa ajili ya uchaguzi wa ndani ya chama hapo mwakani, ni muhimu tukafahamiana wenyewe kwa kina... tunawahitaji viongozi wanaokijua na kukitetea chama chetu.

### KUFAHAMIANA ZAIDI

Katibu wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM mkoani Tanga, Elisante Msuya, anasema mkakati wa kuyaimarisha mashina ya chama hicho, wana-CCM wanapaswa kujitathimini na kutambuana ili kuwabaini wanaokijua na kukitetea chama hicho kwa dhati.

"Tunapojipanga kwa ajili ya uchaguzi wa ndani ya chama hapo mwakani, ni muhimu tukafahamiana wenyewe kwa kina... tunawahitaji viongozi wanaokijua na kukitetea chama chetu," anasema.

Katika ziara hiyo, ujumbe wa Chongolo ulibaini changamoto kadhaa zinazopaswa kufanyiwa kazi na serikali katika ngazi tofauti, ili kufanikisha azma ya kuzitatua.

Miongoni mwa changamoto hizo ni mwingiliano wa huduma za kibinadamu kwenye hifadhi za Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), uboreshaji wa miundombinu katika sekta ya elimu, upungufu wa watumishi hasa kwenye maeneo ya vijijini.

Nyingine ni upatikanaji vifaa na dawa za binadamu kwa kiwango kisichokidhi mahitaji ya wananchi kutokana na wingi wao, migogoro ya ardhi na uhitaji wa kurejesha mashamba yasiyoendelezwa, ili yatumiwe na wananchi kwa kilimo na uwekezaji mwingine.

Katika kushughulikia changamoto hizo na nyinginezo, Chongolo anaahidi kuzifuatilia kwa kina, kupitia wizara za kisekta, atakapotoa mapendekezo yenye nguvu za kuchagiza kasi ya kuzishughulikia na kuzipatia ufumbuzi wa kudumu.

***Mwandishi wa makala haya ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni mkoani Tanga.***
***Mawasiliano 0754-691540, mgeta2000@yahoo.com.***

JUKWAA LA UONGOZI

KENETH KAUNDA

# Aliheshimu demokrasia ya vyama vingi, lakini...



Kenneth Kaunda (kushoto) akisalimiana na hasimu wake kisiasa, Fredrick Chiluba enzi ya uhai wao. Mwingine ni aliyewahi kuwa Rais wa Malawi, Rupiah Banda. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

HISTORIA inaonyesha kuwa Zambia ilipata uhuru mwaka 1964, huku Rais wa kwanza akiwa ni Kenneth Kaunda (97), maarufu KK, aliyeiongoza nchi hiyo kwa miaka 27 chini ya chama cha kijamaa cha United National Independence Party (UNIP).

Uongozi wake ulihitimishwa Oktoba 31 mwaka 1991, baada uchaguzi mkuu wa kwanza ndani ya mfumo vyama vingi, ambaoo ilikipa ushindi chama cha Movement for Multi-Party Democracy MMD cha Fredrick Chiluba.

KK alikuwa anakabiliwa shinikizo linaloongezeka kutoka ndani ya Zambia na duniani kuanzisha demokrasia ya kweli, na hakuwa na jinsi ila kulazimika kukubaliana na kile ambacho dunia inataka.

Kwa mazingira hayo, nchi ilifanya uchaguzi, huku Chiluba, akiibuka mshindi, ambapo Kaunda aliheshimu matokeo ili demokrasia ichukue mkondo wake ingawa inaelezwa bado alikuwa na ushawishi mkubwa nchini mwake.

> Kaunda ametangulia mbele za haki baada kuishi miaka 97 ambayo Mungu alimjalia kuwa hapa duniani, huku akiwa ameacha alama kwa kuheshimu demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Pamoja na kwamba baada ya kushindwa katika uchaguzi huo aliheshimu matokeo ili demokrasia ya vyama vingi iendelee kushamiri, alijikuta katika wakati mgumu baada ya serikali mpya kumkamata na kumshtaki kwa uhaini.

Si kushtakiwa tu, bali serikali hiyo ya Rais Chiluba, ilikuwa na mkakati wa kutaka kumtangaza kuwa ni mtu ambaye si raia wa Zambia, lakini baadaye mahakama nchini humo ikautupilia mbali.

### CHANZO CHA HAYO

Pamoja na kuanguka katika uchaguzi ndani ya mfumo wa vyama vingi na kuheshimu matokeo, inasemekana KK alikuwa bado ni ushawishi kwa Wazambia, hali uliosababisha serikali mpya kumuona kama tishio.

Mwaka 1996 ulitokea uaasi wa baadhi ya wanajeshi uliosababisha wakamatwe huku Kaunda naye akituhumiwa kuhusika na kuwekwa ndani, hali iliyosababisha mkongwe huyo wa siasa za Afrika kulalamika.

Kutokana na kesi hiyo alidai kubambikiwa, hadi kufikia kugoma kula chakula na kupaza sauti ya kupinga kufanya njama hizo huku akishiniza kuachiwa huru na serikali ya hasimu wake huyo ambaye naye kwa sasa ni marehemu.

Hatua ya kugoma kula, ilisababisha swahiba wake wa karibu, Mwalimu Nyerere kufunga safari hadi jijini Lusaka kumbembeleza ale chakula huku shinikizo la kutaka awe huru likiendelea.

Ushawishi wa Nyerere ulisaidia kumfanya akubali, wakala naye chakula katika chumba alichokuwa amefungiwa, huku shinikizo la kimataifa la kuitaja serikali kumwachia huru likiendelea na hatimaye akaachiwa.

Juhudi zote za serikali ya Rais Chiluba za kutaka kumbana Kaunda asifurukute zilikwama baada ya shinikizo la kimataifa, hivyo akawa huru na kuendelea na maisha hadi wiki iliyopita alipofariki dunia.

Nyerere na Kaunda walikuwa ni marafiki wakubwa ambao walishirikiana na viongozi wengine wengi katika harakati za ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika kuzitoa kwenye makucha ya makaburu.

Hivyo, ushirikiano wao katika harakati hizo za ukombozi ziliwafanya wawe karibu, na hata Kaunda alipokumbana na mizengwe hiyo, Nyerere alilazimika kumtembelea na kumtia moyo.

Urafiki wa Mwalimu Nyerere na baadhi ya viongozi akiwamo Kaunda 'KK' ulimaanisha urafiki katika kuikomboa Afrika uliohusisha vyama vya ukombozi kama ZANU-PF, ANC, SWAPO na FRELIMO, vilihifadhiwa nchini.

### ALIKOTOKEA SIASA

KK alizaliwa Aprili 28, 1924 katika kituo cha wamishonari karibu na mpaka baina ya Rhodesia Kaskazini (Zambia ya sasa) na Congo.

Aliwahi kuwa katibu mkuu wa vuguvugu la Northern Rhodesian African National Congress ambalo lilishindwa kuwahamasisha Waafrika dhidi ya shirikisho tawala la wazungu la Federation of Rhodesia na Nyasaland.

Hata hivyo hakukata tamaa, kwani alikuwa mmoja wa viongozi waasisi wa Afrika mpya, kwani kufikia mwaka 1960 alikuwa amekuwa kiongozi wa chama kipya cha United National Independence Party (UNIP).

Aliendelea na harakati hadi Zambia ilipoondokana na ukoloni na kuwa taifa huru, na alisifiwa kama kiongozi aliyekuwa na msukumo wa kisasa katika bara licha ya kwamba mwanzoni aliikataa dhana ya demokrasia ya vyama vingi.

Lakini kutokana na shinikizo la magharibi, alilazimika kuruhusu nchi hiyo kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi, ndipo mwaka 1991 Zambia ikafanya uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo huo.

Uchaguzi huo ndiyo uliomuweka pembeni mzee Kaunda kwenye siasa za Zambia baada kushindwa na kuamua kuruhusu demokrasia ichukue mkondo wake lakini akakumbana na mizengwe ya kuwekwa ndani.

### MWISHO WAPIGANIAUHURU

Kifo cha KK kimeendelea kupunguza idadi ya viongozi walioshiriki katika ukombozi kusini mwa Afrika, huku baadhi ya walishatangulia mbele ya haki wakiwa ni Mwalimu Nyerere na Robart Mugabe wa Zimbabwe.

Wengine ni Samora Machel wa Msumbiji, Agostino Neto wa Angola na wengine kadhaa ambao mchango wao ulikuwa mkubwa katika kuhakikisha nchi zote za kusini mwa Afrika zinakuwa huru.

Kaunda ametangulia mbele za haki baada kuishi miaka 97 ambayo Mungu alimjalia kuwa hapa duniani, huku akiwa ameacha alama kwa kuheshimu demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Katika kundi la viongozi wakongwe wa ukombozi kusini mwa Afrika, Kaunda alikuwa ni miongoni mwa wakongwe waliokuwa wamesalia wakiwamo akina Sam Nujoma wa Namibia, Thabo Mbeki wa Afrika Kusini na wengine wengi.

**MITANDAO**





# Biteko apigia debe vijana fursa madini

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amewataka vijana nchini kuchangamkia fursa zilizoko kwenye sekta za madini ili kuondokana umaskini na utegemezi.

Biteko aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na vijana wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) kwenye mkutano mkuu wa Kongamano la Umoja wa Vijana Taifa uliofanyika jijini hapa mwishoni mwa wiki.

Alisema kwenye sekta ya madini kuna fursa nyingi zinazowasaidia kuondokana na umaskini na utegemezi kwa kuwa ndiyo sekta inayoingizia serikali mapato makubwa.

Pia aliwataka vijana kuhakikisha wanaibua miradi mbalimbali yenye tija ambayo itasaidia kubadili maisha yao kiuchumi.

“Changamoto kubwa iliyopo kwa vijana wengi wanashindwa kufikia malengo yao ni kutokana na aina ya marafiki wanaokuwa nao ambao wengi wao hawana maono yanayoweza kuibua miradi zaidi ya kukatishana tamaa na kujikuta wakisubiri kuwezeshwa,” alisema.

Alisema ili kufikia malengo hayo vijana wanatakiwa kujiepusha na vishawishi ambavyo vinasababisha kutofikia malengo.

Naye Askofu Mkuu wa TAG, Dk. Barnabas Mtokambali, alisema sera ya kanisa hilo ni kuhakikisha waumini wake wakiwamo vijana kufanya kazi kwa bidii kujikwamua kiuchumi.

“TAG hakina chama chochote cha kisiasa ambacho kinachoshabikia, bali kama kanisa kwa upande wao ni walezi wa vyama vyote vya siasa ila waumini wake wapo kwenye vyama hivyo,” alisema.

# Waziri aonya utumikishaji watoto kilimo cha tumbaku

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imepiga marufuku wakulima na kampuni kuwatumia watoto katika uendeshaji wa kilimo cha tumbaku ili kuepuka kushtakiwa kimataifa kama ilivyotokea kwa Malawi.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa wadau wa tumbaku ulioambatana na uzinduaji wa timu itakayoshughulika na uendelezaji wa zao hilo.

Alisema ni kosa kubwa kuwatumia watoto katika kilimo hicho, na kuonya kwamba atakayebainika kuwatumia atachukuliwa hatua za kisheria.

“Nisingependa kuona watoto wanatumika katika kilimo cha tumbaku. Tusije shtakiwa kimataifa kwa sababu sheria hairuhusu watoto kutumiwa katika kilimo hicho,” alisema Bashe.

Alisema hakuna sababu ya kuwatumia watoto bali wafanye wao wenyewe kwa weledi ili kuendeleza kilimo hicho.

Bashe alifafanua kuwa serikali haitopenda kuona kwenye zao hilo kunatokea matatizo yoyote bali wanapaswa kwenda kufanya vizuri kama ilivyo kwenye korosho na mazao mengine ya kimkakati.

Kuhusu upandaji miti, Bashe alisema kuna maeneo mengi ya wazi ambayo wakulima wanapaswa kufanya hivyo ili kulinda ustawi wa kilimo hicho na mazingira.

“Unapolima tumbaku ni lazima uwe na miti ili kutengeneza mazingira ya uboreshwaji wa zao hilo na tumbaku ya Tanzania inashuka kiwango kutokana na kutokuwapo kwa miti,” alisema.

“Tunatakiwa kwenda kupanda miti kwa wingi ili kuboresha mazingira ya zao hilo. Hatuhitaji kurudi nyuma bali tupige hatua,” alisema Bashe.

Alisema kuna maeneo mengi yako wazi katika wilaya ambazo zinazalisha zao hilo, hivyo wachangamkie na upandaji miti kwenye maeneo hayo.

Pia alisema timu ambayo amezindua itakuwa chini ya Mwenyekiti Nyasebwa Chimago ambaye ataungana na wengine ili kuendeleza zao hilo.




Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Utumishi, Dk. Laurean Ndumbaro (katikati), akitoa ufafanuzi wa masuala ya kiutumishi wakati wa kikao kazi cha Wakuu wa Idara za Utawala na Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma kilichofanyika Chuo cha Mipango jijini Dodoma jana. **PICHA: UTUMISHI**

# Sababu kuipaisha kifedha NMB zatajwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

UBUNIFU na uwekezaji katika mifumo ya kisasa, hasa ya kidijitali, kwa Benki ya NMB, ni miongoni mwa vitu vilivyochangia ubora wa kiutendaji na mafanikio makubwa ya kifedha mwaka jana, imeelezwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alimwambia Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, mwishoni mwa wiki jijini hapa, kwenye hafla ya kukabidhi gawio la Sh. bilioni 21.8 kwa serikali.

Alisema mifumo hiyo imekuwa na tija kubwa si tu kwa taasisi hiyo kinara wa faida bali pia kwa serikali, wananchi na uchumi wa taifa kwa ujumla.

“Katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2018, serikali imekusanya mapato yenye thamani ya Sh. trilioni sita kupitia mifumo hiyo ambayo pia ina mchango mkubwa kwenye ufanisi wa NMB kifedha,” alisema.

Aidha, alisema pamoja na serikali kuwa mwanahisa mkubwa kwenye benki hiyo, pia serikali ni mteja mzuri na mdau wakimkakati wa NMB kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali.

“Pamoja na miradi hii, uwekezaji ambao Benki ya NMB imeufanya kwenye teknolojia, unaendelea kuiwezesha benki kuunganisha mifumo yake na taasisi mbalimbaliza serikali na zisizo za kiserikali na hivyo kurahisisha ukusanyaji wa mapato,” alisema.

Zaipuna alibainisha pamoja na kuunganisha mfumo wa malipo ya serikali katika mifumo ya Benki ya NMB, inaendelea kuwekeza kuhakikisha miamala mingine mbalimbali inafanyika kwa njia ya kielekroniki.

“Juhudi hizi zote zinachangia kuleta ufanisi na pia kupunguza gharama za uendeshaji katika ukusanyaji wamapato. Kwa miaka mitatu, 2018 hadi 2020, Sh. trilioni 5.9 zimekusanywa kupitia mifumo ya Benki ya NMB ambayo imeunganishwa na taasisi mbalimbali zilizopo nchini,” alisema.

Serikali, alisema inajivunia mafanikio makubwa ya NMB na kuwa mbia kwenye taasisi hiyo kitu ambacho kinaifanya kupata faida nyingi zenye tija kutokana nauwekezaji wake wa asilimia 31.8.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Mpango aliwataka Watanzania kuhakikisha benki hiyo inazidi kuwa imara kwa kuwa faida zake ni kubwa kwao na taifa kwa ujumla.

“Tunajivunia uwekezaji wetu katika NMB kwani unalipa. Serikali kwa niaba ya wananchi,nchi tunaipongeza NMB kwa kazi inazozifanya kuwahudumia Watanzania na uchumi wa taifa kwa ujumla,” alisema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya NMB, Dk. Edwin Mhede, alisema zaidi ya ubunifu wa kidijitali, siri kubwa ya mafanikio ni wafanyakazi ambao ndiyo silaha kubwa ya benki hiyo.



# Wakulima mpunga wapata mkopo mil. 950/-

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

CHAMA cha Ushirika wa Wakulima wa Mpunga cha Mwanavala (Mwanavala AMCOS), wilayani Mbarali, kimepokea mkopo wa mashine za kisasa za kuvunia mpunga zenye thamani ya Sh. milioni 950.

Mkopo huo umetolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na wakulima hao wamekabidhiwa mashine 15 za kisasa zitakazowasaidia wakulima kuvuna mazao yao kwa haraka na kwa usahihi.

Akikabidhi mkopo huo kwa wakulima juzi, Waziri wa Kilimo, Prof. Adolph Mkenda, alisema mpunga ni zao la pili kwenye kundi la mazao yanayolimwa zaidi nchini likitanguliwa na mahindi.

"Tatizo kubwa kwenye kilimo cha zao hili imekuwa ni pamoja na matumizi ya zana duni za kilimo, mbegu zisizo na ubora na pembejeo nyingine, nafarijika kukabidhi zana hizi maana ni sehemu ya chachu na mabadiliko katika sekta ya kilimo," alisema Prof. Mkenda.

Alisema zana hizo zitawasaidia wakulima wa zao hilo kuvuna kwa wakati na kupunguza kiwango cha upotevu wa mazao ambacho huwa kinatokea kutokana na matumizi ya zana duni.

Alisema mashine hizo ambazo ni pamoja na 'Combined harvesters' zitasaidia kuongezeka kwa uzalishaji kwa maelezo kuwa zaidi ya wakulima 5,000 watanufaika nazo.

Aliipongeza Benki ya TADB kwa kazi nzuri inayofanya kuchagiza mageuzi kwenye sekta ya kilimo nchini kwa kufanya kazi ambayo iliyokusudiwa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TADB, Japhet Justine, alisema mikopo ya matrekta kwenye kilimo pamoja na zana zingine za kilimo zimetolewa kupitia programu ya ushirikiano kati ya TADB na kampuni ya John Deere na LonAgro kwa makubaliano ya utoaji wa mikopo ya riba nafuu.

Alisema riba ya mikopo hiyo haizidi asilimia 12 na itawasaidia wakulima kuzalisha kwa tija na kuwa na uwezo wa kurejesha mikopo yao benki kwa ajili ya wakulima wengine kunufaika.

Justine alisema kuanzia mwaka 2017 hadi sasa, zaidi Sh. bilioni 12 za mikopo imetolewa katika ununuzi wa zana za kisasa za kilimo na kati ya fedha hizo Sh. bilioni 8.3 za mikopo imetolewa moja kwa moja na TADB.

Mkopo huo umenufaisha moja kwa moja wakulima 5,800 katika mikoa ya Katavi, Manyara, Pwani, Kagera, Mwanza, Iringa, Rukwa, Songwe, Njombe, Tanga na Zanzibar.

"Hadi kufikia Juni 8, mwaka huu, TADB ilikuwa imeshatoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 23.3 ambayo imenufaisha wakulima 14,508 katika mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini Sh. bilioni 13.9 ilikuwa mikopo ya moja kwa moja na Sh. bilioni 9.4 zilitolewa kupitia mfuko wa dhamana ya wakulima wadogo (SCGS)," alisema Justine.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Nguvu Kazi ya Mwanavala, Hamza Tamimu, aliishukuru TADB kwa kuwawezesha kupata matrekta ambayo yatachochea kilimo cha mpunga wilayani humo.

Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa maeneo nchini yanayozalisha mpunga kwa wingi inadaiwa hata mapato ya halmashauri hiyo yanategemea zaidi kilimo hicho.



Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Dk. Yahya Msuya (kulia) na baadhi ya watumishi wa halmashauri hiyo, wakikagua moja ya visima vilivyochimbwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), kupitia Mradi wa SAWA katika Zahanati ya Kijiji cha Iwowo, wilayani humo mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya uboreshaji wa Sekta ya Afya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Asimulia uteuzi ulivyomkuta safarini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, Cosmas Nshenye, ameeleza alivyokutana na taarifa za kuteuliwa kwenye nafasi hiyo akiwa safarini kwenda kumwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, kwenye shughuli ya kitaifa jijini Mbeya.

Akizungumza juzi kwenye uzinduzi wa Programu ya kuimarisha mnyororo wa thamani wa mazao ya kahawa, chai, mboga na matunda ijulikanayo Agri-Connect, alisema taarifa ya uteuzi ilimshtua.

Alisema baada ya kuzipata aliamua kusimama kwa muda ili kufuatilia kama bado yumo kwenye orodha ama la ili aendelee na safari au kurudi kwenda kukabidhi ofisi wilayani Mbinga ambako alikuwa anahudumu awali.

Alisema baada ya kuona jina lake limo na amehamishiwa katika Wilaya ya Mbozi, aliamua kuendelea na safari ya kumwakilisha bosi wake wa awali na kuunganisha kwenda kujitambulisha Mbozi.

"Nimekuja hapa kumwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Ibuge, lakini natakiwa niende kujitambulisha Songwe na namwona bosi wangu mpya, Omary Mgumba hivyo nina kila sababu ya kumshukuru Rais wetu Mama Samia kwa kuniamini," alisema Nshenye.

Aliahidi kuwa atahakikisha anashirikiana na viongozi wengine wa Mkoa wa Songwe ili wananchi wapate maendeleo ya kweli na kwamba bahati nzuri ametoka kwenye wilaya inayolima kahawa na nahamia kwenye wilaya nyingine inayolima zao hilo.

Alisema atahakikisha anasimamia zao hilo ili wananchi wazalishe kwa tija na kuongeza kipato kitokanacho na zao hilo pamoja na mazao mengine.

Nshenye alisema katika Wilaya ya Mbinga alisimamia vizuri shughuli za kilimo na kazi zingine za maendeleo na kwamba huenda ni kigezo cha kuendelea kuaminiwa na rais.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mgumba alimtaka kiongozi huyo pamoja na wakuu wa wilaya zote za mkoa huo kusimamia shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao ili kuhakikisha fedha za umma hazipotei.

Mgumba alisema viongozi hao pia wana wajibu wa kukabiliana na matatizo ya lishe kwa wananchi kwa kutoa elimu ili kuondokana na tatizo la udumavu linaloukabili mkoa huo.

"Sisi tumeaminiwa na rais kuja kuwahudumia wananchi wa mkoa huu, sasa ni wajibu wetu kuhakikisha tunawatumikia kisawasawa, lazima tuhakikishe wananchi wanapata huduma wanazostahili, tuhakikishe halmashauri zinatenga asilimia 10 ya mapato kwa ajili ya vikundi vya wajasiriamali," alisema Mgumba.

Vilevile, aliwataka kusimamia mapato ya halmashauri kwa kushirikiana na wakurugenzi hasa kwenye kuziba mianya ya upotevu wa fedha za umma.

# Wahimizwa kuanzisha sungusungu kukabili uhalifu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi wametakiwa kuunda vikundi vya ulinzi shirikishi maarufu sungusungu ili vishirikiane na Jeshi la Polisi kukabiliana na vitendo vya uhalifu vilivyoanza kuibuka katika baadhi ya maeneo ya mji huo.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Mbali, Lusekelo Edward, wakati alipokuwa anazungumza na wananchi kuhusu matukio ya uhalifu yaliyoanza kuibuka kwenye mitaa mbalimbali na kutaka ushirikiano kati ya wananchi na jeshi hilo.

Alisema baadhi ya matukio hayo ni upigaji nondo na uporaji wa mali za wananchi pamoja na uporaji wa pikipiki na mauaji ya waendesha pikipiki hizo.

Alisema viongozi wa mitaa wana jukumu la kutusaidia kuunda vikundi hivyo ili tusaidiane navyo kwenye ulinzi maana kuna maeneo tumeshaanza kuona matunda ya vikundi hivyo.

"Juzi juzi kule Mageuzi sungusungu walimkamata mtu mmoja usiku akiwa na pikipiki ambayo haina funguo na alikutwa na kisu, alipohojiwa hakuwa na majibu ya kueleweka ndipo wakamleta kituoni na tunaendelea kumhoji," alisema Lusekelo.

Aliwataka wananchi pia kuhakikisha wanakuwa makini na mali zao ili kuepuka kukwapuliwa na vibaka na kwamba ikitokea wakakutana na mazingira ya aina hiyo watoe taarifa kwenye mamlaka za kiserikali.

Nao baadhi ya wananchi walilipongeza Jeshi la Polisi kwa kushirikiana nao kwenye kukabili matukio ya uhalifu wakidai kuwa ushirikiano huo utasaidia kumaliza matukio hayo.

Mmoja wa wananchi hao, Goldon Nisakumbona, alisema hata kama vitaundwa vikundi hivyo itahitajika elimu ya kutosha kwa wananchi ili wajue umuhimu wa sungusungu.

Alisema kuna wakati baadhi ya vijana waliokuwa kwenye vikundi vya sungusungu waligeuka kuwa wahalifu hali iliyofanya wananchi kukosa imani na vikundi hivyo.





# Zanzibar yaadhimisha rasmi Siku ya Wajane

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KWA mara ya kwanza Zanzibar inaadhimisha Siku ya Wajane ambayo huadhimishwa kila ifikapo Juni 23.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Taasisi ya Kusaidia Wajane Zanzibar (ZAWIO), Tabia Makame, alisema wakati dunia inaadhimisha siku hiyo, wajane wa Zanzibar wanakabiliwa na matatizo mbalimbali zikiwamo udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Alisema wanawake wajane hasa wale walioachwa na waume zao baada ya ndoa kuvunjika, wengi wao huwa na msongo wa mawazo kutokana na kuelemewa na mzigo wa malezi ya watoto.

Tabia alisema baadhi ya wanaume ndoa zinapovunjika, huwatelekeza watoto wao, hivyo wanawake wajane huangaika na malezi ya watoto bila ya msaada kutoka kwa baba wa watoto wao.

Alisema baadhi ya wanawake wajane Zanzibar wanakabiliwa na wimbi la umaskini, afya duni na umaskini wa kipato hali ambayo husababisha kuhangaika na watoto.

Mkurugenzi huyo pia alisema ZAWIO imejikita katika kuwasaidia kinamama wajane na imekuwa ikiwapa mitaji kwa ajili ya kufanya biashara na kujikimu kimaisha.

Alisema idadi ya wajane Zanzibar inaongezeka kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukosa uvumilivu kwa wanandoa katika ndoa zao.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kuwa na tahadhari kwa uwepo wa baadhi ya taasisi kuwasajili wajane kwa fedha jambo ambalo taasisi yao imekuwa ikipiga vita dhidi ya tukio hilo.

Hivyo, alitumia fursa ya kuwaonya wale wote wanaofanya vitendo hivyo kupitia mgongo wa taasisi hiyo kuacha mara moja.

Naye Mwenyekiti wa TAWIO, Rose Sarwatt, alisema hawafurahii kuwapo ongezeko kubwa la wanawake wajane hivyo aliwataka wanandoa kudumisha ndoa zao.

Kaulimbiu ya mwaka huu ya Siku ya Wajane Duniani "Mapambano Dhidi ya COVID - 19 Wajane Washiriki Kikamilifu - Haki kwa Mama Wajane ni Lazima".

# Tahadhari kali yatolewa dhidi ya ugonjwa corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imetangaza tahadhari nzito dhidi ya maradhi ya corona ikiwamo kuwapima watu wanaoingia na kutoka.

Sambamba na hatua hizo, pia imewataka wananchi kujiepusha na mikusanyiko isiyo ya lazima.

Akitangaza mkakati huo wa kukabiliana na awamu ya tatu ya wimbi la corona, Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema serikali imeamua kuchukua hatua hiyo baada ya nchi jirani kuonekana kuongezeka na baadhi ya huduma kusitishwa.

Alizitaja nchi ambazo zinakabiliwa na ongezeko la ugonjwa wa corona kuwa ni Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Afrika Kusini.

Kutokana na hali hiyo, alisema Zanzibar imeamua kuchukua tahadhari kutokana na baadhi ya nchi hizo kuwa jirani na Tanzania na wananchi wake wamekua wakiingia na kutoka.

"Tuwaomba wananchi wajiepushe na mikusanyiko isiyokuwa ya lazima, kuvaa barakoa, kunawa mikono na kujiepusha kushikana mikono kama njia ya kusalimiana," alisema Mazrui.

Hata hivyo, alisema katika awamu ya tatu ya wimbi la corona, Zanzibar bado iko salama kwa sababu hakuna mgonjwa hata mmoja aliyejitokeza kupitia vituo vya uchunguzi kwa watu wanaoingia na kutoka Zanzibar, wakiwamo watalii kutoka mataifa mbalimbali ya Ulaya na Afrika.

Kuhusu msimamo wa Zanzibar na chanjo ya corona, Waziri Mazrui alisema suala hilo ni la kitaifa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano imeunda kamati ya kitaalamu ya kufuatilia chanjo kabla ya kutoa uamuzi kuhusu kutumika kwa chanjo hiyo baada ya kuthibitika ubora na usalama wake.

"Endapo itathibitishwa kuanza kutumika baada ya kamati kumaliza kazi yake. Mimi nitakuwa wa kwanza kuchanjwa ili kama ina madhara nianze kudhurika. Lakini suala la chanjo litafanyika kwa uwazi na wananchi wataarifiwa rasmi," alisema.

Mazrui alifafanua zaidi kwamba wakati kamati inaendelea kufanyia kazi majukumu iliyopewa na serikali, serikali iko tayari kupokea chanjo ya aina yoyote ya corona, lakini itakuwa tayari kutumia chanjo mpaka serikali ya Jamuhuri ya Muungano itakapotoa msimamo wa pamoja baada ya kamati ya wataalamu kumaliza kazi yake na kuwasilisha ripoti.

Kuhusu msimamo wa Tanzania na suala la chanjo kwa wananchi wake, awali Waziri Mazrui alizikumbusha taasisi zote na maeneo yanayotoa huduma kuzingatia kanuni za wataalamu wa afya juu ya kujikinga na maambukizi ya corona katika maeneo ya huduma wanazotoa.

Kampeni ya kujihadhari na corona inaonekana kushuka kwa kiwango kikubwa tofauti na awali ulipoingia ugonjwa huo, jambo ambalo linahitaji kuhamasishwa kwa nguvu na wataalamu wa afya pamoja na vyombo vya habari.




Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, kuhusu wimbi la tatu la ugonjwa wa corona. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ACT yataka hatua kali waliohusika ubadhirifu wa fedha

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimesema kuvunja bodi kutokana na kashfa za ubadhirifu wa fedha haitoshi bila kuchukuliwa hatua za kisheria viongozi au watendaji waliohusika.

Hayo yalielezwa na Naibu Katibu wa Ngome ya Vijana wa chama hicho, Muhammed Rajab Muabeshi, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya mwelekeo wa uchumi na mpango wa maendeleo ya bajeti ya serikali ya mwaka wa fedha 2021/22 iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Alisema kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), imebainika kuna matumizi holela yasio na marejesho kwa baadhi ya taasisi za serikali na mashirika ya umma huku wahusika wakiachwa bila kuchukuliwa hatua.

"Wizi wa fedha unafanywa bila ya serikali kuchukua hatua ya kuvunja na hatua ya kuvunja bodi hazitoshi, ngome ya vijana ya ACT inashauri waliotajwa na ripoti ya CAG ni lazima wachukuliwe hatua za wazi ili fedha zirejee na wingine wasithubutu," alisema Muhammed.

Aidha, alisema kwamba serikali ifanye uchunguzi dhidi ya meli ya Mapinduzi namba mbili na ichukuliwe hatua dhidi ya watu watakaobainika kuhusika na ubadhirifu au kuhujumu meli hiyo.

Kuhusu hali ya kiuchumi, alisema serikali ya umoja wa kitaifa haijafanya vizuri kutokana na mfumuko wa bei unaondelea kujitokeza tangu serikali ya awamu ya nane kuingia madarakani na kuwaumiza wananchi. "Ukweli wa jambo hili ni kwamba kuna mfumuko mkubwa wa bei za bidhaa tokea serikali hii ingie madarakani kwa mfano mwezi wa Januari dumu la mafuta ya kula lita 20 lilipanda kutoka Sh. 42,000 hadi Sh. 68,000, mafuta ya alizeti lita 10 kutoka Sh. 25,000 mpaka Sh. 32,000, mchele wa basmati kilo 25 kutoka Sh. 49,000 mpaka 56,000 hadi leo," alisema ambaye chama chake kinashiriki kuunda Serikali ya GNU. Aidha, alisema Zanzibar hivi sasa kuna wimbi kubwa la wahamiaji kutoka Tanzania Bara, Kenya, Uganda na kuathiri ajira kwa vijana wa kizanzibari zikiwamo za ulinzi na katika sekta ya utalii baada ya kuchukuliwa na wageni.

Aliongeza, "serikali bado haijataka kudhibiti hili, mashirika yote ya binafsi yameajiri watu kutoka Tanganyika, Kenya, Uganda kwa masikitiko makubwa baadhi ya nafasi zimechukuliwa wakati tunao vijana wetu ambao walipaswa kushika nafasi hizo na kuna wahamiaji ambao sio wazawa wamepewa vitambulisho vya Mzanzibari Mkazi na wamevitumia kujichotea ajira."

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA.35 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZAUSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**SADRUDIN ABDULLA ESMAIL JETHA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**NURJEHAN SADRUDIN ABDULLA ESMAIL JETHA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuninya 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya **tarehe 15th mwezi jull mwaka 2021.**
Imewasilishwa Dar Es Salaam leo tarehe 16th mwezi june 2021.

116320602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA (MCA)63**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**KARABAGAINE WILAYA YA BUKOBA**
**MADAI NAMBA 05 / 2021**

**Mdai- Hamad Adam Kishengeija**
**Mdaiwa- Salim Seif Ndovu**

Salim Seif Ndovu unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii tarehe
28 / 06 / 2021 saa 2.30 asubuhi kuja kujibu madai ukiwa na mashahidi wako kwa kuwa ni siku ya kukata shauri.

Fika na hati zote zianzohusiana na shauri hilo na kama hautahudhuria shauri hili litaendelea upande mmoja.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na mhuri wa mahakama hii

**C.R.RICHARD**
**HAKIMU**
**MAHAKAMA YA MWANZO KARABAGAINE**

116320902

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**BEATRICE DANIEL KITEMI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **SKYMARK SUPER** yenye namba za usajili **MC 613 BJQ** chasis namba **B2INDF07J15001226** enginje namba **B2INDE06D15001226,** yeyote atakayeikota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **MKB/RB/TR/104/2021**

116321002

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Richard Kileo**
**Mkazi wa Majengo Manispaa ya Shinyanga.**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye jina la Tanzania Tea Packers LTD aina ya Nissan Datsun yenye namba za usajili **T. 496 AGC**
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Richard **Kileo kwa simu 0715980680 Rbnamba ShyRb/2021, Control namba 9910824266177.**

116321102

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**FABIAN OSWARD KAZALA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI AINA YA KING LION YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 210 CUR** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/ TR/RB/205/2021**

116321202

---

## DHAMANA YA GARI GARI INAUZWA

**KAPALAMA INTERNATIONAL LIMITED** kwa idhini tuliyopewa na **DAGAA MICROFINANCE LIMITED** tutauza dhamana ya ndugu **ELIZABETH JOHNI MAMBO,** dhamana ya gari yenye namba za usajili **T 281 DQJ** aina ya **TOYOTA PROBOX VAN,**tarehe **27/06/2021**
**Kwa mawasiliano:**
**0714 300 700**
**AU 0768 775 000**

116321502

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AZA GODBLES MLELI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 221 DFX** – TOYOTA NOAH. CHASSIS Na. AZR600105250 ENGINE Na IAZ4308355. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI: **KBA/RB/2268/21.**

1116321602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 117 YA MWAKA 2015**
**BAINA YA**
**WILSON MAGAWA ............................MDAI**
**DHIDI YA**
**PRIDE TANZANIA LIMITED**
**TULVIN INVESTMENT**
**COMPANY.........................WADAIWA**
**BENESTER MATEKERE**

**KWA: PRIDE TANZANIA LIMITED**

**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria **tarehe 12.08.2021 saa 3:00 asubuhi.** Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANAGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hayi ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo **tarehe 18/06/2021**

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

1116321702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Mahakama ya Mwanzo MAKOLE**
**Wilaya ya DODOMA**
**MADAI NAMBARI 50/2021**
**MDAI............................ JANE LUKAMBONA**
**DHIDI YA**
**MDAIWA............FREDRICK HABEL NGOMAI**
**KWA: FREDRICK HABEL NGOMAI**
**DODOMA - NZUGUNI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba
**MADAI YA PESA TSHS. 15,000,000/=**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii **siku ya JUMATATU tarehe 28/6/2021 saa 2:30 asubuhi** kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi *wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama *hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikidhibitisha kama *umepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kwa kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya **Mahakama hii leo 21/06/2021**.

116321802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 119 YA MWAKA 2015**
**BAINA YA**
**STANLEY MAGUNILA ...............MDAI**
**DHIDI YA**
**PRIDE TANZANIA LIMITED**
**TULVIN INVESTMENT**
**COMPANY..................WADAIWA**
**ABUBAKAR ABDALLAH**

**KWA: PRIDE TANZANIA LIMITED**

**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria **tarehe 12.08.2021 saa 3:00 asubuhi.** Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANAGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hayi ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo **tarehe 18/06/2021.**

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

116321902

---

## TANGAZO KUPOTEA KADI YA PIKIPIKI

**Dickson Jorwa Agalla** mkazi wa Ngokolo Manispaa ya Shinyanga. Anatangaza kupotelewa na Kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 215 AVJ** aina ya **LIFAN.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Dickson Jorwa Agalla kwa simu namba **0764157791.** RB namba/ **Shy/RB/2021**, control namba **9910824310488.**

116322002

---

## TANGAZO LA MNADA

**KESI YA TALAKA NA: 55 YA 2020**
**REGINA J SILAHA .........MSHINDA TUZO**
**DHIDI YA**
**ENOCK EVEREST SANGOVA**
**......MSHINDWA TUZO**
Advanced Credit Recovery Co Ltd Kwa amri tuliyopewa Na Mahakama ya Mwanzo Arusha Mjini, tutauza Kwa mnada nyumba iliyoko Njiro Mtaa wa Kalimaji kata ya Moshono
Mnada utafanyika tarehe 25/07/2021 saa 4.00 asubuhi Na kuendelea.

**MASHARTI YA MNADA:**
1: Mnunuzi atalipa asilimia 25% ya bei hapo hapo Na asilimia 75% ilipwe ndani ya siku 14.
2: Ukaguzi wa nyumba utafanyika siku mbili kabla ya mnada .
Endapo mshindi atashindwa kulipa asilia 75% iliyobaki ndani ya muda uliotolewa atakuwa amepoteza haki yake na nyumba itauzwa umpya

**Kwa mawasiliano piga namba:**
**0785132130,**
**0767132130 au Kwa Email:**
**advancedcreditr@gmail.com**
**Imetolewa Na Dalali wa Mahakama**

116322102

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**MICHAEL J.PETER** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki, **TOYO** yenye namba za usajili **MC 659 AUB** na **BOXER** yenye namba za usajili **MC 585 BGT** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/RB/7620/2021.**

116322202

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**EINOTI OBEDI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P.0679-0006** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **KIMANDOLU SEKONDARI** mwaka **2013.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/209569/2021.**

116322602

---

**MOPEH COMPANY LIMITED**
P. O. Box 590., Mob. +255 785 335544, 0713 639979, 0673-335528
E-mail:mopehltd20@gmail.com - Dar es Salaam – TANZANIA.

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na benki ya **Letshego Bank** tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mteja aliyeshindwa kulipa mkopo wake Kama Tarehe ya mnada inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini:

| Na | DHAMANA | JINA LA MDAIWA | ENEO ILIPO | TAREHE | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KIWANJA NA JENGO(GOD OWN) | EMMANUEL. E MAFUE | TANDIKA | 15/07/2021 | SAA 4.30 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa jinsi ilivyo
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 25% ya bei ya mnada ya siku ya mnada na asilimia 75% iliyobakia ilipwe ndani ya siku 14, kinyume na hapo kiasi kilichotolewa hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
3. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa4.30 asubuh hadi saa 10 alasiri.
4. Gharama za kubadili hati ya umiliki (transfer of ownership) ni za mnunuzi.

**KWA MAWASILIANO:**
**Wasiliana na ofisa wa Mopeh Co. Ltd au Fika ofisi za Letshego Bank zilizopo Ursino North, Barabara ya Mwai Kibaki au kwa maelezo zaidi au**
**Piga simu no: 0785 335544.**

116322702

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# EU yaiondolea Burundi vikwazo

**Bujumbura,** BURUNDI

MWAKILISHI wa Umoja wa Ulaya (EU), Claude Boshu, amebainisha kuwa msaada wa euro milioni 430 uliokuwa utolewe kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020, sasa utatolewa baada ya mazungumzo na Rais Evariste Ndayishimiye.

Umoja huo umechukua uamuzi wa kusimamisha vikwazo ilivyoiwekea Burundi tangu mwaka 2015.

Msemaji wa Rais Ndayishimiye alisema rais ameikaribisha hatua hiyo. Baada ya kupokelewa kwa mazungumzo na Rais Evariste Ndayishimiye, mwakilishi wa Umoja wa Ulaya, Burundi, Claude Boshu alisema hatua ya kusimamishwa vikwazo imechukuliwa baada ya wataalamu wa halmashauri mbalimbali kukutana.

"Kwa kauli moja wataalamu kutoka nchi 27 za umoja wa ulaya wameagiza kuondolewa vikwazo vya kusimamisha misaada ya kifedha vilivyowekewa serikali ya Burundi, hii ni hatua kubwa na muhimu kwani miezi sita hadi saba iliyopita msimamo ulikuwa mwingine."

Mwanadiplomasia huyo wa EU, alisema kuwa uamuzi huo ni kufuatia hatua za kuridhisha zilizoazimiwa na rais katika sekta za utawala bora na kuheshimu haki za binadamu.

Na kwamba kuna matumaini ya kuwa katika miezi ijayo hatua nyingine zikaidhinishwa.

Kwa upande wake Evelyne Butoyi, msemaji wa rais alisema Rais Ndayishimiye na mwakilishi huyo wa EU, wamekubaliana juu ya umuhimu wa mikakati imara ya serikali.

"Wamekaribisha ushirikiano ulivyo mzuri kati ya pande hizo mbili, hivyo wameagiza kuzidishwa kwa uwajibikaji kwa kubuni mikakati iliyo imara itakayoiruhusu Burundi kufikia maendeleo endelevu. Na kwamba dhamira ya ushirikiano huo ni kuboresha maisha ya raia."

Msaada wa fedha kwa serikali ya Burundi unaokadiriwa kufikia milioni 430 kwa kipindi hicho, ulisimamishwa na Umoja wa Ulaya na kuitaka serikali kujadiliana na wapinzani walio uhamishoni.

Kigezo hicho kilitupiliwa mbali na serikali ya Burundi, iliyowataja wapinzani hao kama wahusika wa jaribio la mapinduzi yaliyofeli mwaka 2015, na hivyo kuchukuliwa hatua hiyo ya kusimamishwa misaada ya kifedha kwa serikali huku ikiendelea kutolewa misaada ya kiutu.

Tangu Febuari mwaka huu, kumekuwa na majadiliano yanayoendelea kati ya serikali ya Burundi na EU.

EU ni mfadhili mkuu wa Burundi na kurudi kuisaidia kifedha serikali kutaipiga jeki kwenye bajeti ya serikali ambayo tangu kusimamishwa misaada hiyo, imekuwa ikiendeshwa kutumia kodi na ushuru unaotolewa na raia.

**DW**



Maofisa wa uchaguzi wakiendelea kuhesabu kura jana, mjini Addis Ababa, baada ya uchaguzi wa majimbo na mabunge uliofanyika nchini Ethiopia, juzi. Raia wa nchi hiyo wanasubiri matokeo ya uchaguzi mkuu huo. **PICHA: REUTERS**

# Ethiopia wasubiri matokeo uchaguzi wa majimbo

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

RAIA wa Ethiopia, wanasubiri matokeo ya uchaguzi mkuu uliofanyika Jumatatu wiki hii, uchaguzi ambao Waziri Mkuu Abiy Ahmed, amesema utadhihirisha ukomavu wa demokrasia nchini humo.

Uchaguzi huo ni kipimo cha demokrasia katika nchi ya pili kwa idadi kubwa ya watu barani Afrika, inayoongozwa na Waziri Ahmed, mshindi wa tuzo ya Nobel.

Vituo vya kupigia kura vilifungwa saa tatu usiku saa za Afrika Mashariki na kinachoendelea kwa sasa ni kuhesabu kura, na matokeo yanatarajiwa kutangazwa na Tume ya Uchaguzi baada ya siku kadhaa.

Hata hivyo, wakazi wa jimbo lenye mzozo la Tigray na maeneo yenye changamoto za usalama hawakupiga kura na sasa watawachagua wawakilishi wao tarehe sita mwezi Septemba.

Vyama vya upinzani vilivyoshiriki kwenye uchaguzi huu kikiongozwa na kile cha Ethiopian Citizens for Social Justice, vimedai kuwepo kwa udanganyifu kwa madai kuwa mawakala wao wametishwa na kuhitilafiwa kwa masanduku ya kuhifadhi kura.

Wapiga kura milioni 38 waliruhusiwa kushiriki kwenye uchaguzi huo kuwachagua wabunge kati ya wagombea zaidia ya 9,000 waliowania katika majimbo mbalimbali.

**RFI**

## Laurent Gbagbo amtaliki mkewe

**Abidjan,** IVORY COAST

VYOMBO vya habari vya Ivory Coast, vimeripoti kwamba rais wa zamani wa nchi hiyo, Laurent Gbagbo amempa talaka mke wake Simone Gbagbo.

Anachukua hatua siku kadhaa baada ya kurejea katika taifa hilo la Afrika Magharibi, akitokea Ubelgiji.

Katika taarifa iliyochapishwa kwenye tovuti ya kibinafsi, Wakili wa Laurent Gbagbo, Claude Mentenon alisema kuwa Gbagbo alikuwa anataka kumtaliki Simone baada ya kukataa mara kwa mara kwa miaka mingi kukubali kuachana naye.

Simone kwa sasa ni Naibu Mwenyekiti wa Chama cha Laurent Gbagbo cha Ivorian Popular Front (FPI).

Wote wawili, walishtakiwa na Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) kwa uhalifu unaohusiana na mzozo, uliotokea baada ya uchaguzi wa mwaka 2010 na 2011, ingawa walikutwa bila hatia na kuachiliwa huru.

Wakati mumewe alipokuwa Ubelgiji, mara kwa mara Simone aliunga mkono na kutoa wito wa kurejea kwake nchini.

**BBC**

## China kuisaidia Congo Brazzaville kwa mkopo

**Brazzaville,** CONGO

CHINA imekubali kuliangazia upya deni la taifa la Congo Brazaville, Waziri wa Fedha, Rigobert Roger, amesema hatua hiyo itasaidia pakubwa, kupatikana mkopo kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF).

Hatua hiyo imeafikiwa baada ya Rais Denis Sassou Nguesso, kufanya mazungumzo na mwenzake wa CHina, Xi Jinping.

Taarifa zilisema mazungumzo kati ya viongozi hawa wawili yalidumu kama nusu saa, nayo yalijikita juu ya namna ya kuboresha ushirikiano kati ya Brazzaville na Beijing.

Miongoni mwa walioshiriki mazungumzo hayo ni pamoja na Waziri wa Fedha wa Congo Brazzaville Rigobert Roger Andély na pia msaidizi wa rais wa nchi hiyo, vyombo vya habari viliripoti.

Marais hao wawili, walijadili kwa kina kuhusu suala la deni ni chanzo cha kuharibika kwa uhusiano wa nchi hiyo na IMF.

Rais Nguesso ameridhika na matamshi ya mwenyeji wake Xi-Jinping, ambaye ameahidi kufanya kila linalowezekana kuhakikisha mapendekezo ya nchi yake kuhusu deni linalodaiwa taifa hilo na IMF, na ambalo limedumu kwa muda mrefu.

Mvutano wa IMF na Congo-Brazzaville uliibuka baada ya dunia kushuhudia mlipuko wa janga la corona, huku mataifa mengi kujikuta katika ugumu wa kuinua uchumi na kushindwa kulipa deni la IMF.

**RFI**

## ATLETICO WATAJA DAU KUMWACHIA TRIPPIER



**MADRID, Hispania**

MABINGWA wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Atletico Madrid, wameweka wazi dau litakalomfanya Kieran Trippier kuruhusiwa kuondoka hapo kwenye dimba la Wanda Metropolitano.

Trippier anahusishwa na Manchester United ambapo kwa siku za karibuni, kulikuwa na taarifa kuwa klabu hiyo imewakatalia kumwachia mlinzi huyo baada ya kutoa ofa ya pauni milioni 30.

Miamba hao wa LaLiga wameweka wazi kuwa timu yoyote inayomtaka Trippier, itapaswa kupeleka dau la pauni milioni 43, tofauti na hapo hawatakuwa tayari kumuachia.

United wapo sokoni kumtafuta beki wa pembeni atakayechuana na Aaron Wan Bissaka kuanzia msimu ujao.

Ukiachilia mbali Trippier, United pia inahusishwa na Max Aarons wa Norwich City ambaye walimkosa wakati wa dirisha la usajili wa dirisha dogo, Januari.



# DEMBELE AONDOLEWA MICHUANO EURO 2020

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Ousmane Dembele, anatarajiwa kukosa mchezo wa mwisho wa Ufaransa wa hatua ya makundi kwenye michuano ya Euro 2020 dhidi ya Ureno leo Jumatano baada ya kuumia goti.

Mchezaji huyo, ambaye aliingia akitokea benchi katika sare ya Jumamosi dhidi ya Hungary, ilibidi achunguzwe uwanjani baada ya kupata majeraha.

Kocha Didier Deschamps alithibitisha baada ya mechi hiyo kwamba ilikuwa jeraha la kifundo cha goti ambalo lingehitaji upimaji na uchunguzi zaidi.

Kwa mujibu wa gazeti la L'Equipe, Dembele atakosa mechi yote iliyosalia katika mashindano ya Euro 2020 na kuna hofu anaweza kuwa nje kwa muda mrefu zaidi.

Ufaransa wanaongoza Kundi F kabla ya mechi ya mwisho ya kundi, lakini wanakabiliwa na mtihani mgumu dhidi ya Ureno ambao walipigwa na Ujerumani mechi ya mwisho.

Vijana wa Joachim Low, Ujerumani wako katika nafasi ya pili na watacheza dhidi ya Hungary leo Jumatano.

## CALHANOGLU SASA KUTUA INTER MILAN

**MILAN, Italia**

HAKAN Calhanoglu atajiunga na Inter Milan mara tu mkataba wake utakapomalizika kule AC Milan mwishoni mwa mwezi huu, kwa mujibu Sky Sports Italia.

Calhanoglu ambaye bado ana mkataba na AC Milan, atatimka klabuni hapo wiki ijayo pale tu mkataba wake utakapokamilika.

Calhanoglu ameitumikia AC Milan kwa miaka minne na alikataa dau la Euro milioni nne lililotolewa na timu hiyo ili kuendelea kuitumikia.

Alijiunga na AC Milan akitokea klabu ya Bayer 04 Leverkusen mwaka 2017 na tangu hapo, amecheza mechi 43 na kutoa pasi za mwisho 12 na kufunga tisa katika michuano yote.

Katika michuano ya Euro 2020, Hakan Calhanoglu amecheza mechi tatu tu na kutoa pasi moja tu ya bao.

Mchezaji mwenye asili ya Ujerumani na Uturuki ameamua kuichezea Uturuki na alikuwa miongoni mwa wachezaji tegemeo wa kikosi hicho.

Usajili huo wa Inter unaelekea kufanya maboresho eneo la ushambuliaji kutokana na tetesi mbalimbali zilizopo kuwa baadhi ya wachezaji wanaweza kuuzwa katika majira haya ya joto.



## HABARI MICHEZO




# STERLING AKIRI KUKOSA FURAHA MAN CITY

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa England, Raheem Sterling, amekiri kwamba, hakuwa na furaha kwa kukosa muda wa kutosha wa kucheza pale Manchester City msimu uliopita.

Sterling amehusishwa na kuondoka kwa mabingwa wa hao wa Ligi Kuu baada ya kukaa benchi mara kadhaa mwishoni mwa msimu wa 2020-21, pamoja na robo fainali na nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amekuwa mtu muhimu kwa England katika mechi zao za ufunguzi za michuano ya Euro 2020, akifunga bao la ushindi dhidi ya Croatia wiki iliyopita.

Akizungumzia hali yake ya soka pale Man City, Sterling amesema kukosa nafasi ya kucheza mara kwa mara kulimfanya kutokuwa na furaha.

"Ikiwa huchezi, huna furaha. Ni mimi, huyo ni mimi tangu nilipokuwa mtoto, ikiwa ninacheza mpira nina furaha sana, ikiwa sichezi sina furaha," alisema akinukuliwa na Daily Mail.



# Varane, United waanza kuteta

**MANCHESTER, England**

WAWAKILISHI wa Raphael Varane wanatarajia kukutana na Manchester United wiki hii kwa matumaini ya kukamilisha uhamisho wake kwenda Ligi Kuu England.

Beki huyo wa kati, ambaye mkataba wake umebaki miezi 12, anaonekana yupo mbioni kusepa pale Real Madrid.

Kwa mujibu wa gazeti la Uingereza la Mirror, Varane hana furaha kule Santiago Bernabeu na waliwachagua wachezaji kama Luka Modric, Lucas Vazquez na Sergio Ramos kuongeza mikataba kabla ya hawajaongea naye.

Na Ligi Kuu England ndiyo inayoonekana kumvutia Varane na Man United ndiyo kituo chake kifuatacho.

Kwa mujibu wa ripoti, Real Madrid wanataka Euro milioni 60 kumuuza mchezaji huyo huku wakitarajia kufanya uhamisho wa fedha kubwa kwa wachezaji kati ya Kylian Mbappe au Erling Haaland.

Paris Saint-Germain pia wanaonekana kuvutiwa na beki huyo, lakini Varane anapenda kwenda England.




# GREALISH SASA ANUKIA KUTIMKA ASTON VILLA

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City imetajwa kwamba, inaandaa kitita kikubwa cha fedha kwa ajili ya kumsajili Jack Grealish kutoka Aston Villa.

Miezi kadhaa iliyopita, Man City walihusishwa sana na kuhitaji saini ya Grealish ambaye amekuwa nyota wa Villa na kufanya vizuri sana kwa msimu huu.

Grealish mwenye umri wa miaka 25, kwa msimu huu uliokamilika ameonyesha kiwango kikubwa sana hali iliyomfanya kuzivutia klabu nyingine kama Manchester United na Man City yenyewe.

Msimu uliopita Grealish alihusishwa sana kujiunga na Man United msimu uliopita, lakini dili hilo halikufanikiwa kutokana na kukosekana kwa fedha za kutosha katika klabu hiyo yenye maskani yake pale Old Trafford.

Aston Villa ina mkataba na Grealish hadi mwaka 2025 na wameweka dau la pauni milioni 100 kwa mchezaji huyo kwa timu yoyote itakayohitaji huduma yake.

Kocha wa Man City, Pep Guardiola ni mnazi mkubwa sana wa Grealish na ametaja jina lake kama kipaumbele cha kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MAN CITY YAWEKA MEZANI PAUNI MIL. 100 KWA KANE

●●●Lakini United, Chelsea, Real Madrid, Barca na PSG nazo zinatia mkono kwa...

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City imetoa ofa maalumu ya pauni milioni 100 ili kumsajili Harry Kane kutoka Tottenham Hotspur, kwa mujibu wa Daily Mail.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England kwa sasa yupo na timu ya taifa kwenye michuano ya Euro 2020.

Kane aliripotiwa kwamba hana furaha katika Klabu ya Tottenham na kwamba anataka kutafuta changamoto mpya na kusaka mataji.

Kwa kipindi chote alichokaa hapo Spurs, hajawahi kutwaa taji lolote na hivyo malengo yake kwa sasa ni kutafuta timu ambayo itamwezesha kubeba mataji.

Wakati akitwaa tuzo ya mchezaji bora wa msimu wa Ligi Kuu England, Kane alinukuliwa akisema kwamba, tuzo binafsi si kipaumbele chake kikubwa, kwani anataka kutwaa mataji na timu

Na sasa kwa mujibu wa ripoti hiyo, Kane anaweza kuondoka kwa miamba hao wa Tottenham kipindi cha majira ya joto na mabingwa wa Ligi Kuu England, Man City ndio wanaotajwa kuwania saini yake.

Man City imeamua kuingiza miguu yote miwili kwa kuwa tayari kutoa ofa ya pauni milioni 100 ili kumsajili.

Hata hivyo, Man City watakabiliwa na changamoto katika mbio hizo, kwani pia Kane anawaniwa na Manchester United, Chelsea, Real Madrid, Barcelona na Paris Saint-Germain.

## KWA UFUPI

**BARCA YAMTAKA RONALDO**

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta ana ndoto ya kuwakutanisha Cristiano Ronaldo na Lionel Messi msimu ujao na yuko tayari kutoa ofa ya wachezaji wawili katika juhudi za kuishawishi Juventus kumuuza mshambuliaji huyo wa Ureno aliye na umri wa miaka 36. ***(AS)***

**JESUS CHAMBO KWA KANE**

KLABU ya Manchester City wako tayari kuwajumuisha, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 24 na Raheem Sterling mwenye miaka 26, katika dau la kumnunua Harry Kane mwenye miaka 27, ambaye Tottenham inakadiria thamani yake kuwa paundi milioni 150. ***(Times)***

**TORRES AKARIBIA UNITED**

MANCHESTER United wamepiga hatua katika juhudi za kumsajili mlinzi wa Hispania, Pau Torres kwenye umri wa miaka 24 kutoka Villarreal. ***(Manchester Evening News)***

**BENITEZ KUTUA EVERTON**

RAFAEL Benitez anakaribia kujiunga na Everton baada ya kufanya mazungumzo zaidi na klabu hiyo wikendi iliyopita, licha ya mashabiki kupinga mpango wa kuteuliwa kwa kocha huyo wa zamani wa Liverpool. ***(Mirror)***

**FAVRE ATAJWA PALACE**

KLABU ya Crystal Palace wamefanya mazungumzo na Lucien Favre kuhusu uwezekano wa kuchukua nafasi ya Roy Hodgson, lakini huenda wakakabiliwa na upinzani kutoka kwa Everton. ***(Guardian)***

**RUDIGER ANOGEWA CHELSEA**

MLINZI wa Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, anataka kusalia Chelsea msimu ujao ingawa klabu hiyo haijaanzisha mazungumzo ya kurefusha mkataba wake wa sasa, unaomalizika msimu ujao. ***(Sky Sports)***

**DUMFRIES AGOMBEWA ULAYA**

BAYERN Munich wameungana na Everton, AC Milan na Inter Milan katika mbio za kuwania saini ya mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi, Denzel Dumfries mwenye umri wa miaka 25, kutoka PSV Eindhoven. ***(Voetbal International)***

**SOUMANRE KUTUA LEICESTER**

KIUNGO wa kati wa Lille na Ufaransa, Boubakary Soumare mwenye umri wa miaka 22, atafanyiwa uchunguzi wa afya pale Leicester katika kipindi cha siku 10 zijazo kabla ya kusaini mkataba wa miaka mitano na klabu hiyo ya Ligi ya Kuu England. ***(La Voix des Sports)***

**LIVERPOOL KUMUUZA TSIMIKAS**

LIVERPOOL hawana mpango wa kumuuza, Kostas Tsimikas msimu huu wa majira ya joto licha ya mlinzi huyo wa Ugiriki aliye na umri wa miaka 25, kucheza mara saba pekee katika kikosi cha kwanza msimu uliopita. ***(Liverpool Echo)***

**ROMA WANAMTAKA PATRCIO**

AS Roma wanajadiliana na Wolves kuhusu kipa Rui Patricio mwenye umri wa miaka 33, kwa sababu klabu hiyo ya Ligi Kuu England inataka kumnunua kwa kati ya dau la paundi milioni 10 na 13. ***(Sky Sports)***

**WARD AWANIWA WOLVES**

KLABU ya Wolves inataka kumsajili kipa wa Leicester na Wales, Danny Ward mwenye umri wa miaka 27, ambaye ameonyesha umahiri wake katika michuano inayoendelea ya Euro 2020. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO

# AZAM YAVULIA KOFIA KIWANGO NAMUNGO

Na Adam Fungamwango

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, ameisifu timu ya Namungo FC, akisema kuwa waliwapa tabu na kuziba mianya yote hadi kuamua kumuingiza Never Tegere kwa ajili ya mipira faulo.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mjini Lindi na timu hizo kutoka suluhu, kocha huyo raia wa Burundi alisema kutokana na jinsi walivyocheza, Namungo waligundua kuwa isingekuwa rahisi sana kupata bao kwa njia ya kupigiana pasi, hivyo waliamua kuwawekea mtego wa faulo ambao nao ulishindikana.

"Haikuwa mechi nyepesi. Namungo ni timu nzuri, baada ya muda tuliona kupata bao kwa njia ya kawaida ni ngumu. tukamuingiza Never Tegere kwa sababu yeye ni mzuri sana kwa mipira ya faulo. Tuliona hiyo ndiyo njia pekee ambayo ingeweza kusababisha kupata bao," alisema kocha huyo.

Hata hivyo, alisema ni kama vile Namungo pia walijua hilo, nao wakapunguza kucheza faulo kwenye maeneo ya hatari.

"Kwa bahati mbaya kama na wao waliona hatari inayowakabili mbele. Hawakucheza faulo kwenye maeneo ya hatari kama tulivyokuwa tunatarajia, lakini tunashukuru tu hata kwa pointi hii moja ambayo tumeipata, tutaendelea kupigana kwenye mechi zilizobaki hadi mwisho wa ligi ndiyo tutajua nafasi yetu," alisema.

Kocha Mkuu wa Namungo Hemed Morocco, alizisifu timu zote mbili kwa kucheza vizuri na wao kutengeneza nafasi nyingi kuliko wapinzani wao, lakini wachezaji wake walishindwa kuzitumia.

"Tulizitaka sana pointi tatu ili kupigania nafasi ya nne twende tena kimataifa, lakini tumeshindwa. Hata hivyo tutapambana kwenye mechi zilizobaki ili kuisaka tena nafasi hiyo," alisema.

Namungo ipo nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 43, Azam ikiwa nafasi ya tatu kwa pointi zake 64.

PAMOJA SANA...



Mmoja wa viongozi wa wanaumoja wa Klabu ya Namanga Jogging, Michael Juma, akiongoza mazoezi ya viungo baada ya kushiriki mbio za taratibu wakati wa bonaza lililoandaliwa na klabu hiyo na kushirikisha klabu zaidi ya 10 katika viwanja vya Namanga, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KMC, Mtibwa Sugar wafurahia sare

Na Adam Fungamwango

MATOKEO ya sare ya bao 1-1 kati ya KMC FC na Mtibwa Sugar juzi kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, yamepokewa kwa furaha na makocha wa timu hizo.

Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Mohamed Badru, amesema ilikuwa washinde mechi hiyo, lakini walifanya kosa moja lililosababisha KMC wasawazishe, lakini amefurahishwa na sare hiyo kwa sababu timu yake ilikuwa ugenini.

"Kiufundi ni kwamba tulifanya kosa moja lililotugharimu, vinginevyo tungetoka na ushindi. vijana wangu walikuwa wazito kushambulia kwa haraka. Sisi huwa tunashambulia tukiwa watano, lakini tulishindwa kupata matokeo kwa sababu hiyo, na pia KMC ni timu ngumu," alisema Badru.

Kocha huyo alisema kucheza saa nane pia kuliwaathiri kwa sababu kuna baadhi ya wachezaji wake walichoka sana na kulazimika kufanya mabadiliko ili kuingiza wenye pumzi.

"Kusema kweli wachezaji wangu wamepambana na nimeridhika na sare niliyoipata," alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa KMC, Habib Kondo, alisema mchezo ulikuwa wa kibabe na ufundi mkubwa kiasi kwamba sare ilikuwa ni halali kwa timu zote.

"Lengo letu la kwanza ilikuwa ni kushinda. Walipotufunga bao ilibidi tubadilishe mbinu ya uchezaji ili tupate angalau sare. Kwenye mechi hii tumebadilisha mfuno wa uchezaji mara tatu. Nimeridishwa kabisa na sare," alisema.

Kwa matokeo hayo, KMC inafikisha pointi 42, ikiwa kwenye nafasi ya sita ya msimamo wa Ligi Kuu, huku Mtibwa Sugar ikiwa nafasi ya 10 kwa pointi 38 ilizokuwa nazo mpaka sasa.

## Waogeleaji chipukizi kushindana Julai 3

Na Mwandishi Wetu

JUMLA ya klabu sita za mchezo wa kuogelea zimethibitisha kushiriki katika mashindano ya waogeleaji chipukizi (Junior Championships) yaliyopangwa kufanyika kwenye Bwawa la Kuogelea la Gymkhana jijini Dar es Salaam Julai 3-4, mwaka huu.

Katika mashindano hayo ambayo yatashirikisha waogeleaji wenye umri wa miaka 12 na kushuka chini, klabu ambazo zimeshathibitisha kushiriki ni Dar es Salaam Swimming Club (DSC), Bluefins, Taliss, FK Blue Marlins, Lake Swim Club na Mis Piranhas.

Katibu Mkuu wa Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA), Inviolata Itatiro, amesema mwisho wa klabu kuthibitisha ushiriki wao ni kesho na kuziomba ambazo hazijathibitisha kufanya hivyo mapema.

Alisema mashindano hayo mpaka sasa yamepata udhamini wa Kilombero Sugar Company Limited na Tanga Fresh huku akitoa wito kwa kampuni nyingine kufanya hivyo.

"Tunawaomba wadhamini wengine wajitokeze ili kufanikisha mashindano haya muhimu kwa maendeleo ya mchezo wa kuogelea nchini. Kuna gharama mbalimbali ikiwa pamoja na uendeshaji wa mashindano pia, si kazi rahisi kufanywa na TSA, tunaomba wadau wasaidie," alisema Inviolata.

## Tano zafuzu robo fainali FA Cup Znz

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU tano tayari zimefuzu hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) maarufu FA Cup, inayoendelea visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya ZFF ambaye ni mratibu wa michuano hiyo, Haji Issa Kidali, alizitaja timu ambazo zimeshafuzu hatua hiyo kuwa ni KMKM, JKU, Polisi, Kundemba FC na Kilimani City.

Kidali alisema michuano hiyo inaendelea kwa upande wa Unguja pekee huku kisiwani Pemba ikiwa haijachezwa huku akifafanua kuwa hali hiyo haiwezi kuathiri lolote.

Alisema kwa mujibu wa kanuni ya mashindano hayo msimu huu, bingwa wa FA Kanda ya Unguja atakutana na yule wa Kanda ya Pemba ili kupata timu moja itakayoiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# Michezo

Jumatano Juni 23, 2021

Nipashe




MAN CITY YAWEKA MEZANI PAUNI MIL. 100 KWA KANE

HABARI UK 22




Romelu Lukaku akiitendea haki pasi ya mwisho kutoka kwa Kevin De Bruyne kwa kuifungia Ubelgiji bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Finland kwenye michuano ya Euro 2020 iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Krestovsky, Saint Petersburg nchini Urusi. **PICHA: MTANDAO**

# SARPONG, DUBE SHIDA FA CUP YANGA, AZAM

## ●●●Zatangulia Tabora, Songea kuzisubiri Simba, Biashara United lakini...

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga na Azam FC, zikiondoka jijini Dar es Salaam kuelekea Tabora na Songea tayari kwa kuwasubiri wapinzani wao kwenye mechi ya hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup, zina shida katika safu zao za ushambuliaji kutokana na kukabiliwa na majeruhi kwa nyota wao muhimu, imeelezwa.

Yanga itavaana na Biashara United keshokutwa, Ijumaa katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora wakati Jumamosi Azam ikiwa na shughuli pevu kwenye Dimba la Majimaji mjini Songea dhidi ya Simba.

Hata hivyo, Yanga ambayo imeondoka leo alfajiri kwa ndege kuelekea Tabora tayari kwa mchezo huo, katika safu yake ya ushambuliaji itamkosa Michael Sarpong lakini ikikosa huduma ya baadhi ya nyota wangine wakiwamo Yassin Mustapha na Shaibu Abdallah 'Ninja'.

Kwa upande wa Azam FC, hatima ya Prince Dude, kuwa sehemu ya kikosi kitakachocheza dhidi ya Simba Jumamosi, iko mikononi mwa daktari wa timu hiyo kutokana na mshambuliaji huyo kusumbuliwa na tumbo.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema maandalizi ya kikosi chake kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya yapo vizuri.

Alisema itakuwa mechi ngumu na wanaenda kupambana kuhakikisha wanapata matokeo ya ushindi ili kusonga mbele na kucheza fainali ya michuano hiyo.

"Tunapambana kutafuta matokeo katika Ligi Kuu, lakini tunahitaji kushinda katika mchezo wa nusu fainali ili tucheza fainali na kutwaa taji hilo ambalo litatuwezesha kushiriki moja ya michuano ya kimataifa," alisema Nabi. Alisema kulingana na mabadiliko ya kikosi cha timu hiyo, ana imani kubwa ya kufanya vizuri licha ya kutambua mchezo huo utakuwa mgumu huku akiwakosa baadhi ya wachezaji wake hao ambao ni majeruhi.

"Hakuna mechi itayokuwa rahisi kwetu, tuna waheshimu wapinzani wetu, nimeandaa timu yangu kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri katika mechi zetu zijazo ikiwamo mchezo wetu huu wa nusu fainali dhidi ya Biashara United," alisema Nabi.

Lakini Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, akimzungumzia Dube, ambaye amekosa mechi mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kushindwa kumaliza dakika 90 wakati wakicheza dhidi ya Rhino Rangers, kwenye mchezo wa robo fainali ya FA Cup uliopigwa Uwanja wa Kambarage, Shinyanga kutokana na kuugua tumbo ghafla, alisema nyota huyo ameanza mazoezi mepesi na suala la kuucheza dhidi ya Simba, wanasuburi ripoti ya daktari.

Alisema baada ya kuumwa gafla tumbo alipewa matibabu huku akiendelea kutumia dawa na amerejea kikosini kuendelea na majukumu yake lakini daktari ndiye atakayeamua kumruhusu kocha amtumie ama la.

"Tumejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo wetu dhidi ya Simba, suala la kucheza kwa Dube bado mapema kulisema hilo kwa sababu tunasubiri ripoti ya daktari kutueleza utayari wa nyota huyo kutumika katika mchezo huo," alisema kocha huyo huku akieleza kuwa wanatarajia kuondoka Dar es Salaam leo kwa ndege kuelekea Songea tayari kwa mchezo huo.

# DEMBELE AONDOLEWA MICHUANO EURO 2020



**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Ousmane Dembele, anatarajiwa kukosa mchezo wa mwisho wa Ufaransa wa hatua ya makundi kwenye michuano ya Euro 2020 dhidi ya Ureno leo Jumatano baada ya kuumia goti.

**UK. 20**

# VARANE, UNITED WAANZA KUTETA




**MANCHESTER, England**

WAWAKILISHI wa Raphael Varane wanatarajia kukutana na Manchester United wiki hii kwa matumaini ya kukamilisha uhamisho wake kwenda Ligi Kuu England.

**UK. 21**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002